Food and Agriculture
Organization of the
United Nations

# Mwongozo Wa Hiari Kuhusu Uwajibikaji Katika Usimamizi Wa Umiliki Wa Ardhi, Maeneo Ya Uvuvi Na Misitu Kwa Ajili Ya Upatikanaji Na Uhakika Wa Chakula Kwa Taifa



CFS
Committee on
World Food
Security

# Mwongozo Wa Hiari Kuhusu Uwajibikaji Katika Usimamizi Wa Umiliki Wa Ardhi, Maeneo Ya Uvuvi Na Misitu Kwa Ajili Ya Upatikanaji Na Uhakika Wa Chakula Kwa Taifa

SHIRIKA LA CHAKULA NA KILIMO LA UMOJA WA MATAIFA

Kenya, 2021

Required citation:
FAO. 2021. *Mwongozo Wa Hiari Kuhusu Uwajibikaji Katika Usimamizi Wa Umiliki Wa Ardhi, Maeneo Ya Uvuvi Na Misitu Kwa Ajili Ya Upatikanaji Na Uhakika Wa Chakula Kwa Taifa*. Kenya.

The designations employed and the presentation of material in this information product do not imply the expression of any opinion whatsoever on the part of the Food and Agriculture Organization of the United Nations (FAO) concerning the legal or development status of any country, territory, city or area or of its authorities, or concerning the delimitation of its frontiers or boundaries. The mention of specific companies or products of manufacturers, whether or not these have been patented, does not imply that these have been endorsed or recommended by FAO in preference to others of a similar nature that are not mentioned.

The views expressed in this information product are those of the author(s) and do not necessarily reflect the views or policies of FAO.

© FAO, 2012 [English edition]
© FAO, 2021 [Swahili edition]]

ISBN 978-92-5-134532-0
© FAO, 2021

Some rights reserved. This work is made available under the Creative Commons Attribution-NonCommercial-ShareAlike 3.0 IGO licence (CC BY-NC-SA 3.0 IGO; https://creativecommons.org/licenses/by-nc-sa/3.0/igo/legalcode).

Under the terms of this licence, this work may be copied, redistributed and adapted for non-commercial purposes, provided that the work is appropriately cited. In any use of this work, there should be no suggestion that FAO endorses any specific organization, products or services. The use of the FAO logo is not permitted. If the work is adapted, then it must be licensed under the same or equivalent Creative Commons licence. If a translation of this work is created, it must include the following disclaimer along with the required citation: “This translation was not created by the Food and Agriculture Organization of the United Nations (FAO). FAO is not responsible for the content or accuracy of this translation. The original English edition shall be the authoritative edition.”

Disputes arising under the licence that cannot be settled amicably will be resolved by mediation and arbitration as described in Article 8 of the licence except as otherwise provided herein. The applicable mediation rules will be the mediation rules of the World Intellectual Property Organization http://www.wipo.int/amc/en/mediation/rules and any arbitration will be conducted in accordance with the Arbitration Rules of the United Nations Commission on International Trade Law (UNCITRAL).

**Third-party materials.** Users wishing to reuse material from this work that is attributed to a third party, such as tables, figures or images, are responsible for determining whether permission is needed for that reuse and for obtaining permission from the copyright holder. The risk of claims resulting from infringement of any third-party-owned component in the work rests solely with the user.

**Sales, rights and licensing**. FAO information products are available on the FAO website (www.fao.org/publications) and can be purchased through publications-sales@fao.org. Requests for commercial use should be submitted via: www.fao.org/contact-us/licence-request. Queries regarding rights and licensing should be submitted to: copyright@fao.org.

# Yaliyomo


Shukrani ..... iv
Dibaji ..... v

1 Utangulizi ..... 1

1. Malengo ..... 1
2. Mawanda ya Matumizi ..... 2

2 Masuala ya Jumla ..... 3

3. Kanuni zinazoongoza Uwajibikaji katika Usimamizi wa Umiliki wa Ardhi ..... 3
3A. Kanuni za jumla ..... 3
3B. Kanuni za utekelezaji ..... 4
4. Haki na wajibu wa Umiliki ..... 5
5. Sera, Sheria na Miundo inayohusu Umiliki: ..... 7
6. Utoaji wa Huduma ..... 9

3 Utambuzi wa Kisheria na Ugawaji wa Hakimilki na Wajibu ..... 12

7. Ulinzi wa hakimiliki ..... 12
8. Ardhi ya Umma, Maeneo ya Uvuvi na Misitu ..... 13
9. Jamii Asilia, Wazawa, na Jamii Nyingine Zenye Mifumo ya Umiliki wa Kimila 15
10. Umiliki Usiorasmi ..... 17

4 Uhamisho na Mabadiliko Mengine ya Hakimiliki na Wajibu ..... 19

11. Masoko ..... 19
12. Uwekezaji ..... 20
13. Kuunganisha Vipande vya Ardhi na Njia Zingine za Marekebisho ..... 24
14 Urejeshaji wa Hakimiliki ..... 25
15. Mabadiliko ya Ugawaji ..... 26
16. Utwaaji Ardhi na Fidia ..... 28

5 Usimamizi wa Miliki ..... 30

17. Kumbukumbu za hakimiliki ..... 30
18. Uthamini ..... 31
19. Utozaji Kodi ..... 32
20. Udhibiti wa Maeneo Yanayopangwa ..... 33
21. Utatuzi wa Migogoro ya Hakimiliki ..... 34
22. Masuala ya mipaka ya kimataifa ..... 35

6 Kukabaliana na Mabadiliko ya Tabianchi na Dharura ..... 36

23. Mabadiliko ya Tabianchi........................................................................................ 36
24. Majanga asilia.................................................................................................... 36
25. Migogoro Inayohusiana na Umiliki wa Ardhi, Maeneo ya Uvuvi na Misitu ...... 38

7 Ukuzaji, Utekelezaji, Ufuatiliaji na Tathmini ...................................................... 40

# Shukrani

Tafsiri hii ya Kiswahili ya Mwongozo wa hiari kuhusu uwajibikaji katika usimamizi wa umiliki wa ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu kwa ajili ya upatikanaji na uhakika wa chakula kwa taifa, imewezekana kutokana na juhudi za watu mbalimbali. Tunawashukuru wote waliohusika kwa kujitolea kwao ili watumiaji wa Kiswahili wapate fursa ya kusoma na kutumia mwongozo huu. Tunawashukuru Maafisa wa Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa, Dkt. Mackay Rigava, Dkt. Wordsworth Larbi, Husna Mbarak na Beatha Fabian, kwa uongozi na usimamizi wao katika mradi huu. Tafsiri hii imefanywa na Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA)-Tanzania, imehaririwa na Profesa Kimani Njogu, na kuidhinishwa na mashirika mbalimbali na Wizara za Ardhi za Kenya na Tanzania chini ya usimamizi wa Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa. Tunawashukuru nyote kwa juhudi zenu zitakazochangia katika usimamizi wa umiliki wa ardhi, maeneo ya uvuvi, na misitu

Tunatoa shukrani za dhati kwa Umoja wa Ulaya kwa ufadhili kupitia programu mbili kuu: Programu ya Usimamizi wa Umiliki wa Ardhi, Kenya, na Programu ya Kimataifa ya Mradi wa Ardhi Kimtambuko.

# Dibaji

Mwongozo huu wa hiari umekusudiwa kama rejeleo na kutoa maelekezo ya kuboresha umiliki wa ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu. Lengo lake kuu ni kufikia uhakika wa chakula kwa wote na kuunga mkono hatua zinazopigwa za haki ya chakula cha kutosha kwa kuzingatia muktadha wa kitaifa wa uhakika wa chakula.

Lengo la Mwongozo huu ni ni kuunga mkono juhudi za kitaifa na kimataifa katika kutokomeza njaa na umaskini, kwa kuzingatia misingi ya maendeleo endelevu na kwa kutambua umuhimu wa ardhi katika maendeleo na kwa kuhimiza haki salama za umiliki na usawa katika kutumia ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu.

Kutokomeza njaa na umaskini, na matumizi endelevu ya mazingira, kunategemea kwa kiwango kikubwa namna watu, jamii na wengine wanavyoweza kuwa na uwezo wa kupata na kutumia ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu. Maisha ya watu wengi, hususan maskini wa vijijini, yanategemea upatikanaji kwa usawa na udhibiti wa rasilimali hizi. Hivi vyote ni vyanzo vya chakula na makazi; msingi wa shughuli za kijamii, kiutamaduni na kidini; na kigezo kikuu katika ukuaji wa uchumi.

Ni muhimu kutambua kwamba uwajibikaji katika kumiliki ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu hauwezi kutenganishwa na upatikanaji na usimamizi wa maliasili nyinginezo, kama vile maji na rasilimali za madini. Kwa kutambua uwepo wa miundo na mifumo tofauti ya usimamizi wa maliasili zilizopo chini ya muktadha wa kitaifa, Serikali zinaweza kuzingatia umiliki wa rasilimali hizi katika utekelezaji wa Mwongozo huu, kwa kadri inavyofaa.

Namna watu, jumuiya na wengineo wanavyoweza kupata na kutumia ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu hufafanuliwa na kusimamiwa na jamii kupitia mifumo ya umiliki. Mifumo hii ya umiliki huamua nani anayeweza kutumia rasilimali gani, kwa muda gani, na kwa masharti gani. Mifumo inaweza kutegemeana na sera na sheria zilizoandikwa, pamoja na desturi na taratibu ambazo hazijaandikwa.

Mifumo ya umiliki wa ardhi inazidi kukumbana na matatizo kutokana na idadi ya watu kuzidi kuongezeka na kuhitaji uhakika wa chakula, na papo hapo uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi hupunguza upatikanaji wa ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu. Hali ya upungufu na kukosekana uhakika wa haki za umiliki wa ardo inaongeza hatari, njaa na umaskini, na inaweza kusababisha migogoro na uharibifu wa mazingira pale inapotokea watumiaji wenye masilahi yanayokinzana wanagombania udhibiti wa rasilimali hizi.

Usimamizi wa umiliki wa ardhi ni kipengele muhimu katika kuamua namna watu, jamii na wengineo wanavyoweza kupata haki, na wajibu unaohusiana na haki hizo, katika kutumia na kudhibiti ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu. Matatizo mengi ya umiliki hutokea kwa sababu ya usimamizi dhaifu, na jitihada za kukabiliana na matatizo ya umiliki wa ardhi huathiriwa na aina ya utawala. Utawala duni huathiri utulivu wa jamii, matumizi endelevu ya mazingira, uwekezaji na ukuaji wa kiuchumi.

Watu wanaweza kuwa na maisha ya njaa na umaskini ikiwa watapoteza haki zao za kumiliki nyumba, ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu kwa sababu ya vitendo vya rushwa katika umiliki au pale asasi za utekelezaji zitashindwa kulinda haki zao za umiliki. Watu wanaweza hata kupoteza uhai wao endapo usimamizi hafifu wa umiliki wa ardhi utasababisha migogoro yenye mapigano. Usimamizi bora wa ardhi kwa upande mwingine unachangia maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi yanayoweza kusaidia kutokomeza umaskini na uhaba wa chakula, na kuhamasisha uwekezaji madhubuti.

Katika kukabiliana na mahitaji makubwa na yaliyotandawaa, FAO na washirika wake walianza mchakato wa kuandaa miongozo kuhusu uwajibikaji katika usimamizi wa umiliki wa ardhi. Hatua hizi zimeunga mkono Mwongozo wa Hiari wa Kuwezesha Hatua za Kufikia Haki ya Chakula cha Kutosha Katika Muktadha wa Kitaifa wa Usalama wa Chakula (Mwongozo Kuhusu Haki ya Kupata Chakula), uliopitishwa na Baraza la FAO katika Mkutano wake wa Mia Moja na Ishirini na Saba (127)- mnamo Novemba 2004, na Mkutano wa Kimataifa Kuhusu Mabadiliko ya Kilimo na Maendeleo Vijijini (ICARRD) wa mwaka 2006.

Katika Mkutano wake wa Thelathini na Sita (36) Mwezi Oktoba 2010, Kamati ya Usalama wa Chakula Duniani (CFS) ilihimiza kuendelezwa kwa michakato jumuishi katika kutengeneza Miongozo hii kwa lengo la kuwasilishwa kwa ajili ya majadiliano na CFS, na kuamua kuanzisha kikosi kazi cha wazi katika CFS ili kuitathmini rasimu ya kwanza ya Miongozo.

Mwongozo huu unaendana na muundo wa nyenzo zingine za hiari za FAO ambazo zinaweka misingi na viwango vinavyokubalika kimataifa kwa kuhimiza uwajibikaji, yaani: *Mwongozo wa Hiari Kuhusu Haki ya Chakula; Kanuni ya Maadili kuhusu Uvuvi wenye Uwajibikaji; Kanuni ya Maadili ya Kimataifa ya Usambazaji na Matumizi ya Viuatilifu; Usimamizi wenye Uwajibikaji wa Misitu ya Kupandwa: Miongozo ya Hiari; na Mwongozo wa Hiari kuhusu Udhibiti wa Moto: Kanuni na Hatua za Kimkakati.* Nyenzo hizi – ambazo bado hazijafasiriwa kwa Kiswahili kwa sasa - ni nyaraka ndogo zinazotoa mifumo inayoweza kutumika wakati wa kuandaa mikakati, sera, sheria, programu na hatua za utekelezaji. Zinatumika kwa pamoja na nyaraka zingine za ziada, kama vile miongozo ya ziada ambayo hutoa maelezo ya kitaalamu juu ya masuala maalumu pale inapolazimu, vifaa vya mafunzo na uhamasishaji, na miongozo mingine ya kusaidia wakati wa utekelezaji.

Mwongozo huu ulipitishwa na CFS katika Mkutano (maalumu) wa thelathini na nane tarehe 11 Mei, 2012. Miongozo hii iliandaliwa na kikosi kazi cha wazi kupitia vikao vya mwezi Juni, Julai na Oktoba 2011 na Machi 2012. Inaendana na mikutano ya mashauriano iliyokuwa jumuishi ndani ya mwaka 2009-2010. Mikutano ya mashauriano ya kikanda ilifanyika Brazil, Burkina Faso, Ethiopia, Jordan, Namibia, Panama, Romania, Shirikisho la Urusi, Samoa na Vietnam. Mikutano hiyo ya mashauriano ya kikanda ilikusanya takribani watu 700, kutoka nchi 133, wakiwakilisha sekta za umma na za binafsi, asasi za kiraia na wanazuoni. Mikutano ilifanyika katika makundi manne, na ilifanyika maalumu kwa ajili ya asasi za kiraia za Afrika (nchini Mali); za Asia (nchini Malaysia); za Ulaya na Asia ya Kati na Magharibi (nchini Italia); na Amerika Kusini (Brazil), ilihudhuriwa na watu takribani 200 kutoka nchi 70, na Mkutano wa ziada wa sekta binafsi ulikusanya watu zaidi ya 70 kutoka nchi 21. Miongozo hii pia inajumuisha mapendekezo yaliyotolewa kupitia ushauri wa

kielektroniki juu ya rasimu ya awali. Mapendekezo ya kuboresha rasimu ya awali yalipokelewa kutoka kwa sekta za umma na za kibinafsi, asasi za kiraia na wanazuoni, na kutoka sehemu mbalimbali duniani.

Mwongozo huu unaendana na nyenzo za kikanda na za kimataifa, ikiwa ni pamoja na Malengo ya Maendeleo ya Milenia, ambayo yanashughulikia haki za binadamu na haki za umiliki wa ardhi. Wakati wasomaji wa Miongozo hii wakitafuta namna ya kuboresha usimamizi wa umiliki wa ardhi, wanahimizwa kufanya mapitio ya mara kwa mara ya nyenzo hizo kwa ajili ya wajibu wao na mikataba ya hiari, na kupata mwongozo wa ziada.

# Sehemu ya Kwanza 1

## Utangulizi

### 1. Malengo

### 1.1 Mwongozo wa Hiari

Miongozo[1] hii inalenga kuweka misingi ya kuboresha usimamizi wa kumiliki ardhi[2], maeneo ya uvuvi na misitu. Kwa kufanya hivyo inatarajiwa kuyanufaisha makundi yote, na hasa watu walio katika mazingira magumu, waliotengwa kwa namna mbalimbali na jamii, kwa nia ya kuhakikisha upatikanaji wa chakula na hatua za kufikia haki ya kupata chakula cha kutosha, kuondoa umaskini, kuwa na maisha endelevu, jamii imara, uhakika wa makazi, maendeleo ya maeneo ya vijijini, utunzaji wa mazingira, jamii endelevu pamoja na maendeleo ya kiuchumi. Ni muhimu programu zote pamoja na sera, misaada ya kitaalamu ya kuboresha usimamizi wa umiliki wa ardhi kupitia utekelezaji wa miongozo hii kufungamana na masharti yaliyopo ya uwajibikaji kwa mataifa chini ya sheria za kimataifa ikiwa ni pamoja na Azimio la Haki za Binadamu na makubaliano yaliyopo katika nyenzo zingine zinazohusiana na haki za binadamu.

### 1.2 Malengo ya Miongozo

1. kuboresha usimamizi wa umiliki kwa kuandaa mwongozo na taarifa kuhusu uzoefu wa mifumo iliyokubalika kimataifa katika kushughulikia haki za watumiaji, usimamiaji na udhibiti wa ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu.

2. kuchangia uboreshaji na uendelezaji wa sera, sheria na mifumo ya kishirika inayodhibiti aina mbalimbali za hakimiliki zilizopo kwenye rasilimali hizi.

3. kuongeza uwazi na kuboresha utendaji wa mifumo ya umilikaji.

4. kuimarisha uwezo na utendaji wa wakala; mamlaka za kimahakama; serikali za mitaa; mashirika ya wakulima na wazalishaji wadogo; jamii za wavuvi; na

[1] Miongozo hii inamaanisha makundi matatu ya mwongozo wa Umilikaji. Makundi haya ni ya (i) ardhi (ii) maeneo ya uvuvi na (iii) misitu

[2] Hakuna ufafanuzi wa kimataifa wa dhana ya ardhi katika muktadha wa umilikaji. Kwa hivyo, mataifa yanaweza kuifafanua dhana hii kutegemea muktadha wa nchi. Katika Mwongozo huu tunapotumia 'umiliki' katika suala la usimamizi tunakusudia umiliki wa ardhi, maeneo ya uvuvi, na misitu

watumiaji wa misitu; wafugaji; jamii za kiasili na jamii zingine; asasi za kiraia; sekta binafsi; wanazuoni; na watu wote wanaohusika na usimamizi wa umiliki; na vilevile kuhamasisha ushirikiano miongoni mwa wadau waliotajwa.

## 2. Mawanda ya Matumizi

### 2.1 Miongozo hii ni ya hiari

2.1 Miongozo hii inapaswa kutafsiriwa na kutumika sawasawa na matakwa ya sheria zinazohusika za kitaifa na kimataifa, na kwa kuzingatia maridhiano ya hiari baina ya nyenzo za kikanda na kimataifa. Miongozo hii ni ya ziada na inaunga mkono juhudi za kitaifa, kikanda na kimataifa zinazoshughulikia haki za binadamu na kutoa haki za kumiliki ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu pamoja na juhudi za kuboresha usimamizi wake. Hakuna chochote katika miongozi hii kinacholenga kuzuia au kudhoofisha majukumu yoyote ya kisheria yanayoihusu nchi kwa mujibu wa sheria ya kimataifa.

2.2 Miongozo hii inaweza ikatumiwa na nchi; wakala za utekelezaji; mamlaka za kimahakama; serikali za mitaa; vyama vya wakulima na wazalishaji wadogo; wavuvi na watumiaji wa misitu; wafugaji; watu wa asilia na jamii zingine; asasi za kiraia; sekta binafsi; wanazuoni; na watu wote wanaohusika kutathmini utawala wa miliki na kuainisha maboresho na kuyatumia.

2.3 Mawanda ya matumizi ya miongozo hii inahusisha dunia nzima. Kwa kuzingatia muktadha wa nchi, miongozo inaweza kutumiwa na nchi na kanda zote katika hatua za ukuaji wa uchumi na kwa ajili ya usimamizi wa mifumo yote ya miliki, ikijumuisha umiliki wa umma, binafsi, jumuiya, pamoja, na kimila.

2.4 Miongozo hii inapaswa kutafsiriwa na kutumika kwa kuzingatia mifumo ya sheria ya kitaifa pamoja na taasisi zake.

# Sehemu ya Pili 2

## Masuala ya Jumla

Sehemu hii inaainisha namna ya kushughulikia masuala ya usimamizi wa umiliki wa ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu kwa kuzingatia haki na wajibu; será; sheria na mifumo ya kishirika; na utoaji wa huduma.

Katika muktadha wa usimamizi wa umiliki, nchi zinawajibika chini ya nyenzo za haki za binadamu za kimataifa. Sehemu hii ya pili inapaswa kusomwa sambamba na aya ya 2.2.

## 3. Kanuni zinazoongoza Uwajibikaji katika Usimamizi wa Umiliki wa Ardhi

### 3A. Kanuni za jumla

3.1 Serikali zinapaswa:

1. Kutambua na kuheshimu wamiliki halali wenye haki na haki zao. Serikali zinapaswa kuchukua hatua stahiki za kutambua, kurekodi na kuheshimu umiliki halali wa wamiliki na haki zao, bila kujali kama zimewekwa kwenye kumbukumbu rasmi au vinginevyo; kuepuka ukiukwaji wa haki za umiliki za wengine; na kukidhi wajibu kuhusiana na haki za umiliki.

2. Kulinda haki za umiliki halali dhidi ya vitisho na ukandamizaji. Serikali zinapaswa kuwalinda wamiliki halali wenye haki dhidi ya hasara zisizotarajiwa kuhusiana na hakimiliki, zinazojumuisha kuondolewa kwa nguvu kunakokiuka utaratibu uliopo wa sheria za kitaifa na kimataifa.

3. Kuhamasisha na kuwezesha manufaa yanayotokana na hakimiliki halali. Serikali zinapaswa kuchukua hatua madhubuti kuhamasisha na kuwezesha upatikanaji wa hakimiliki au kusimamia shughuli mbalimbali zinazohusiana na haki hiyo, kama vile kuhakikisha huduma zinawafikia watu wote.

4. Kuwezesha upatikanaji wa haki katika kushughulikia ikiukwaji wa umiliki halali. Serikali zinatakiwa kuweka njia zenye ufanisi na zinazofikika na kila mmoja, kupitia mamlaka za kimahakama au taratibu nyingine, katika kusuluhisha migogoro inayohusiana na umiliki wa ardhi na kuweka njia zinazofikika na kutekelezeka kwa haraka. Serikali zinapaswa kutoa fidia kwa haki na kwa haraka kwa ardhi inayomilikwa kihalali pale ambapo itachukuliwa kwa manufaa ya umma.

5. Kuzuia kuibuka kwa migogoro, mapigano na rushwa kuhusiana na umiliki. Serikali zinapaswa kuchukua hatua madhubuti za kuzuia kuibuka na kukua kwa migogoro hadi kusababisha mapigano. Vilevile, Serikali zinapaswa kuzuia rushwa katika ngazi zote na katika mazingira yoyote.

3.2 Wadau wasio wa kiserikali, zikiwemo asasi za kibiashara, wanawajibika kuheshimu haki za binadamu na umiliki halali. Asasi za kibiashara zinapaswa kufanya shughuli zao kwa uadilifu ili kuepuka ukiukwaji wa haki za binadamu na umiliki halali wa watu wengine. Pia zinapaswa kuweka mifumo madhubuti ya kukabili vihatarishi ili kuzuia na kutatua madhara makubwa yanayohusiana na haki za binadamu na umiliki halali. Asasi za kibiashara zinapaswa kushiriki na kuweka mifumo isiyo ya kimahakama ili kuzuia madhara, ikiwa ni pamoja na mifumo madhubuti ya kiutendaji inayoshughulikia malalamiko, hususan pale ambapo asasi hizi zimesababisha au kuchangia madhara yenye athari kubwa ya haki za binadamu na umiliki halali. Vilevile, hazina budi kutambua na kutathmini madhara halisi au yanayoweza kutokea juu ya haki za binadamu na umiliki halali endapo zitahusika. Kwa kuzingatia majukumu ya kimataifa, Serikali zinapaswa kuandaa msaada sahihi wa kisheria kwa ajili ya kushughulikia madhara yanayosababishwa na asasi za kibiashara juu ya haki za binadamu na umiliki halali. Pale ambapo mashirika ya ndani na ya kimataifa yatakapokuwa yamehusika, serikali zao zitawajibika kusaidia mashirika hayo na mataifa wenyeji kuhakikisha kwamba biashara hazikinzani na haki za binadamu na umiliki halali wa ardhi. Serikali zinapaswa kuchukua hatua za ziada kulinda dhidi ya ukiukwaji wa haki za binadamu na hakimiliki halali unaofanywa na asasi za kibiashara zinazomilikiwa au kuendeshwa na Serikali au zinazofadhiliwa kwa kiasi kikubwa na kupokea huduma kutoka kwa wakala za Serikali.

### 3B. Kanuni za utekelezaji

Kanuni hizi za utekelezaji ni muhimu katika kuunga mkono uwajibikaji katika usimamizi wa umiliki wa ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu.

1. **Utu:** Kutambua usawa na haki za binadamu wote ambazo haziwezi kuporwa.

2. **Kutokubaguliwa:** Mtu yeyote hapaswi kubaguliwa kwa mujibu wa sheria, sera na utendaji.

3. **Usawa na haki:** Kutambua kwamba usawa baina ya watu unaweza kuhitaji kukubali tofauti baina ya watu na kuchukua hatua chanya ikiwemo uwezeshaji ili kuhamasisha haki sawa za umiliki na upatikanaji wa ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu, kwa wote, wanawake na wanaume, vijana na watu waishio katika mazingira magumu katika muktadha wa kitaifa.

4. **Usawa wa kijinsia:** Kuhakikisha haki sawa kwa wanawake na wanaume katika kufurahia haki zote za binadamu huku zikitambua tofauti baina ya wanawake na wanaume na kuchukua hatua mahususi zinazolenga kuendeleza usawa halisi pale inapobidi. Serikali zinapaswa kuhakikisha kwamba wanawake na wasichana wana haki sawa za umiliki na upatikanaji wa ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu bila kujali hali zao za kiraia na ndoa.

5. **Mifumo jumuishi:** Kutambua kwamba maliasili na matumizi yake yanahusiana, na kwamba ipo haja ya kutafuta mbinu shirikishi na endelevu katika usimamizi.

6. **Ushauri na ushiriki:** Kushirikisha na kutafuta uungwaji mkono wa wale wenye umiliki halali, ambao wanaweza kuathiriwa na uamuzi kabla ya uamuzi kufikiwa kwa sababu wana haki ya umiliki, na mwitikio; kwa kuzingatia uwiano kinzani wa kimamlaka baina ya pande mbalimbali zinazohusika na kuhakikisha ushiriki wa watu na makundi ulio kamilifu, huru, wenye ufanisi, wenye maana na weledi katika mchakato unaohusiana na kufanya uamuzi.

7. **Utawala wa Sheria:** Kufuata mfumo wa kikanuni kupitia sheria zilizotungwa kwa kiasi kikubwa katika lugha zinazotumika kwa wote, zinazotekelezwa kwa usawa bila kuingiliwa, na zinazoshabihiana na matakwa yaliyo chini ya sheria za kitaifa na kimataifa, na kwa kuzingatia matamko ya hiari chini ya nyenzo za kikanda na kimataifa.

8. **Uwazi:** Kufafanua kwa uwazi na kutangaza kwa mapana sera, sheria nataratibu zinazohusika katika lugha zinazofaa, na katika mfumo unaoweza kufikiwa na wote.

9. **Uwajibikaji:** Kuwawajibisha watu binafsi, mashirika ya umma na asasi zisizokuwa za serikali kwa matendo na maamuzi yaokulingana na kanuni za utawala wa sheria.

10. **Uboreshaji endelevu**: Serikali zinapaswa kuboresha taratibu za usimamizi, ufuatiliaji na uchambuzi wa utawala wa umilikaji ardhi ili kuendeleza mipango yenye msingi wa kiushahidi na uboreshaji endelevu.

## 4. Haki na wajibu wa Umiliki

4.1 Serikali zinapaswa kuhakikisha utawala bora wa umiliki kwa sababu ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu ni vya msingi katika kufanikisha upatikanaji wa haki za binadamu, uhakika wa hifadhi ya chakula, uondoaji umaskini, maisha endelevu, utulivu wa kijamii, usalama wa makazi, maendeleo ya vijijini, maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

4.2 Serikali zinapaswa kuhakikisha matendo yote yanayohusu haki na utawala wake yanaendana na matakwa yaliyopo chini ya sheria za kitaifa na kimataifa kwa kuzingatia matamko ya hiari kwa mujibu wa nyenzo zitumikazo kikanda na kimataifa.

4.3 Pande zote zinapaswa kutambua kwamba hakuna umiliki, hata umilikaji binafsi, usiokuwa na masharti. Hakimiliki zote zinapimwa kwa mizani ya haki za wengine na hatua muhimu zinazochukuliwa na serikali kwa matumizi ya umma. Hatua hizo zinapaswa kutokana na sheria kwa malengo ya kukuza ustawi wa jumla ikiwa ni pamoja na kulinda mazingira sambamba na matakwa ya Serikali juu ya haki za binadamu. Pia umiliki unaambatana na wajibu. Pande zote zinapaswa kuheshimu ulinzi wa muda mrefu na utumiaji endelevu wa ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu.

4.4 Kwa kuzingatia tathmini ya hakimiliki sambamba na sheria za nchi, serikali zinapaswa kuweka utaratibu wa kisheria wa kutambua hakimiliki halali ambazo hazijalindwa na sheria zilizopo. Sera na sheria zinazolinda haki za umiliki hazipaswi kubagua na zizingatie jinsia. Pamoja na kanuni za kushauriana na ushirikishwaji wa miongozo hii, Serikali haina budi kufafanua kupitia kanuni zilizosambazwa kwa upana aina za haki zinazoaminika kuwa halali. Aina zote za umiliki zinapaswa kuwapa watu wote kiwango cha usalama wa umiliki kinachowahakikishia usalama wa kisheria dhidi ya kufukuzwa ambako ni kinyume na wajibu wa sheria za kitaifa na kimataifa, na dhidi ya manyanyaso na vitisho vingine.

4.5 Serikali zinapaswa kulinda haki halali za umiliki, na kuhakikisha kuwa watu hawafukuzwi kiholela na kwamba haki zao halali za umiliki hazizimwi au kukiukwa.

4.6 Serikali zinapaswa kuondoa na kuzuia aina zote za ubaguzi zinazohusu hakimiliki ikiwa ni pamoja na zile zinazotokana na mabadiliko ya hali ya ndoa, kukosa uwezo wa kisheria, na kutoweza kufikia rasilimali za kiuchumi. Serikali zinapaswa hususan kuhakikisha haki sawa za umilikaji kwa wanawake na wanaume, ikiwa ni pamoja na haki ya kurithi na kurithisha haki hizi. Hatua hizi za Serikali zinapaswa kuendana na wajibu uliopo chini ya sheria zilizopo za kitaifa na za kimataifa, na kwa kuzingatia kwa matamko ya hiari yaliyopo katika nyenzo zinazohusika za kikanda na kimataifa.

4.7 Endapo kwa jitihada zao wenyewe watu hawawezi kupata haki ya kumiliki ili kujikimu, kuzifikia huduma zinazotokana na taasisi za utekelezaji na mamlaka za kisheria, au kushiriki katika michakato inayoweza kuathiri hakimiliki zao, Serikali zinapaswa kutoa msaada usio wa kibaguzi na unaozingatia jinsi.

4.8 Haki za binadamu zinamhusu kila mmoja, hazigawanyiki, zinahusiana na kutegemeana. Hivyo, usimamizi wa umiliki za ardhi, maeneo ya uvuvi na

misitu havipaswi kuunganishwa moja kwa moja na upatikanaji na utumiaji wa ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu pekee, bali pia haki za kiraia, kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni. Kwa kufanya hivyo, Serikali zinapaswa kuheshimu na kulinda haki za kiraia na kisiasa za watetezi wa haki za binadamu ikijumuisha haki za binadamu za wakulima wadogo, watu asilia, wazawa, wavuvi, wafugaji na wafanyakazi wa vijijini. Aidha, Serikali zinapaswa kutambua matakwa ya haki za binadamu wakati zinaposhughulika na mtu mmoja mmoja na vikundi vinavyolinda ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu.

4.9 Serikali zinapaswa kuweka mfumo wa haki na madhubuti wa kisheria na kiutawala kwa ajili ya kutatua migogoro ya hakimiliki kwa wakati na kwa gharama nafuu. Mifumo hii itajumuisha njia mbadala za utatuzi wa migogoro hiyo na zitaweka suluhu madhubuti zitakazohusisha haki ya kukata rufaa kadiri itakavyofaa. Suluhu hizo zitalazimika kutekelezwa kwa umakini na zitaweza kuhusisha urejeshaji, malipo, na fidia kutokana na uharibifu au hasara. Serikali zitatakiwa kujitahidi kuhakikisha kwamba makundi na watu walio katika mazingira magumu wanaweza kuzifikia njia hizo kwa mujibu wa kifungu cha 6.6 na 21.6. Serikali zihakikishe kuwa mtu yeyote ambaye haki zake zimekiukwa katika muktadha wa haki anazifikia njia za utatuzi wa migogoro na suluhu.

4.10 Serikali zinapaswa kupokea na kuwezesha kushiriki kwa watumiaji wa ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu ili kuwa na ushiriki kamilifu katika mchakato shirikishi wa utawala wa miliki. Vivyo hivyo, uundaji na utekelezaji wa sera, sheria na maamuzi juu ya maendeleo ya nchi kwa jinsi itakavyofaa kwa majukumu ya watendaji wa Serikali na wasio wa kiserikali, kwa mujibu wa sheria na taratibu za kitaifa.

## 5. Sera, Sheria na Miundo inayohusu Umiliki:

5.1 Serikali zinapaswa kuandaa sera, kutunga sheria na kuweka mifumo ya uwajibikaji katika umiliki wa ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu. Mifumo hiyo inategemea na kuwezeshwa, na mabadiliko makubwa ya mfumo wa sheria, huduma za jamii na mamlaka za kimahakama.

5.2 Serikali zinapaswa kuhakikisha kwamba sera, sheria na miundo ya uwajibikaji wa umiliki vinaendana na majukumu yaliyopo chini ya sheria za kitaifa na kimataifa na kuzingatia matamko ya hiari chini ya nyenzo zinazotumika kikanda na kimataifa.

5.3 Serikali zinapaswa kuhakikisha kwamba sera, sheria na miundo ya uwajibikaji wa umiliki inatambua na kuheshimu, kwa mujibu wa sheria za nchi, haki ya umiliki halali, zinazojumuisha hakimiliki halali za kimila ambazo kwa sasa hazilindwi na sheria. Vilevile, serikali zinatakiwa

kuwezesha, kuimarisha na kulinda utumiaji wa hakimiliki. Mifumo inapaswa kusharabu umuhimu wa ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu katika hali ya kijamii, kiutamaduni, kiuchumi na kimazingira. Serikali zinapaswa kuandaa mifumo isiyo ya kibaguzi na kuimarisha usawa wa kijamii na kijinsia. Mifumo inapaswa kusharabu uhusiano uliofungamana baina ya ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu pamoja na matumizi yake, na kuanzisha utaratibu jumuishi kwenye usimamizi wa maliasili hizo.

5.4 Serikali zinapaswa kuzingatia vikwazo mahususi vinavyowakabili wanawake na wasichana kuhusiana na kumiliki pamoja na hakimiliki, na kuchukua hatua kuhakikisha kwamba mifumo ya kisera na kisheria inatoa ulinzi kamili kwa wanawake. Aidha, Serikali zinapaswa kuhakikisha kwamba sheria zinazotambua hakimiliki za wanawake zinatekelezwa na kusimamiwa. Serikali zinapaswa kuhakikisha kwamba sheria zinawawezesha wanawake kuingia katika mikataba inayohusu hakimiliki kwa misingi ya usawa na wanaume. Vilevile, wanawake wanapaswa kupewa huduma za kisheria na misaada mingine ili kuwawezesha kulinda masilahi yao ya kumiliki.

5.5 Serikali zinapaswa kuandaa sera, sheria na taratibu mwafaka kwa njia ya michakato shirikishi inayohusisha pande zote zitakazoathiriwa na kuhakikisha kwamba wanaume na wanawake wanashirikishwa tangu hatua za awali. Aidha, sera, sheria na taratibu zinapaswa kuzingatia uwezo wa Serikali katika kuzitekeleza, na zinapaswa kujumuisha mbinu zinazozingatia jinsia, zinazoelezeka katika lugha nyepesi na zitangazwe kwa mapana.

5.6 Serikali zinapaswa kugatua madaraka ya utelekezaji kwenye ngazi mbalimbali za Serikali zinazoweza kutoa huduma kwa wananchi kwa ufanisi mkubwa. Aidha, Serikali zinapaswa kuainisha kwa uwazi majukumu na wajibu wa Wakala za Serikali zinazohusika na umiliki wa ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu. Vilevile, Serikali zinapaswa kuhakikisha kuwepo kwa uratibu wa shughuli zinazotekelezwa na wadau mbalimbali kama wakala za serikali, serikali za mitaa, watu wa asilia na jamii zingine zenye mifumo ya umiliki wa kimila.

5.7 Serikali zinapaswa kuainisha na kuweka wazi fursa za asasi za kiraia, sekta binafsi na wanazuoni zitakazochangia kuandaa na kutekeleza sera, sheria na mifumo ya kiutawala.

5.8 Serikali na wadau wengine wanapaswa kurejelea na kufuatilia sera, sheria na mifumo ya utawala ili kuendeleza ufanisi. Taasisi zinazotekeleza na mamlaka za mahakama zinapaswa kushirikiana na asasi za kiraia, wawakilishi wa watumiaji na umma kwa ujumla ili kuboresha huduma na kuongeza jitihada za kuzuia ufisadi kupitia michakato ya wazi na utoaji wa uamuzi. Taarifa kuhusu mabadiliko na athari zake zinazotarajiwa ziainishwe na kujulikana kwa upana katika lugha nyepesi.

5.9 Serikali zinapaswa kutambua kwamba sera na sheria za haki miliki zinafanya kazi katika muktadha wa kisiasa, kisheria, kijamii, kiutamaduni, kidini, kiuchumi na kimazingira. Pale ambapo muktadha mpana utabadilika na mabadiliko ya kumiliki yakahitajika, Serikali zitapaswa kuandaa maridhiano ya kitaifa juu ya mabadiliko yatakayopendekezwa.

## 6. Utoaji wa Huduma

6.1 Kutegemea kuwepo kwa rasilimali, Serikali zinapaswa kuhakikisha kwamba taasisi za utekelezaji na mamlaka za sheria zina uwezo wa watumishi, miundombinu, fedha na aina zingine za uwezo ili kumudu utekelezaji wa sera na sheria kwa wakati, ufanisi na kwa kuzingatia uwiano wa jinsia. Watumishi katika ngazi zote za kiutawala wanapaswa kupata mafunzo ya mara kwa mara na kuajiriwa kwa kuzingatia usawa wa jinsia na kijamii.

6.2 Serikali zinapaswa kuhakikisha kwamba utoaji wa huduma zinazohusu umiliki na usimamizi wake unashabihiana na majukumu yaliyoainishwa katika sheria za kitaifa na kimataifa, na kwa kuzingatia matamko ya hiari chini ya nyenzo zingine za kikanda na kimataifa.

6.3 Serikali zinapaswa kutoa huduma kwa wakati, zinazofikika, na zisizokuwa na ubaguzi ili kulinda haki za kumiliki, kuimarisha, na kuwezesha upatikanaji wa haki hizo, na kutatua mabishano. Vilevile, Serikali zinapaswa kuondoa matakwa ya kisheria na kiutaratibu yasiyo ya lazima na kujitahidi kuzuia vikwazo vinavyohusu hakimiliki. Serikali zinapaswa kufanya mapitio ya huduma zinazotolewa na taasisi za utekelezaji na mamlaka za kisheria, na kufanya maboresho pale inapohitajika.

6.4 Serikali zinapaswa kuhakikisha kwamba taasisi za utekelezaji na mamlaka za mahakama zinahudumia umma kwa ujumla, zikitoa huduma kwa wote, ikiwa ni pamoja na wananchi wanaoishi katika maeneo yasiyofikika kwa urahisi. Huduma zinapaswa kutolewa kwa wakati na kwa ufanisi kwa kutumia teknolojia inayofaa katika mazingira yaliyopo ili kuongeza ufanisi na uwezo wa wananchi kuzifikia. Miongozo ya ndani inapaswa kuandaliwa ili watumishi waweze kutekeleza sera na sheria katika hali inayofaa na thabiti. Taratibu zinapaswa kurahisishwa bila kuhatarisha usalama wa kumiliki au ubora wa haki. Vitendea kazi vinavyoeleweka vinapaswa kuwekwa wazi katika lugha nyepesi na kuwaelewesha watumiaji kuhusu haki na wajibu wao.

6.5 Serikali zinapaswa kuandaa sera na sheria ili kuimarisha, utumiaji wa pamoja, kama ipasavyo, wa taarifa za ardhi na nyinginezo zinazohusu kumiliki ili zitumiwe kwa ufanisi na serikali na taasisi za utekelezaji, watu

asilia, wazawa, na jamii nyingine, asasi za kiraia, sekta binafsi, wanazuoni na umma kwa ujumla. Kuandaliwe viwango vya vya kitaifa kuhusu utumiaji wa taarifa ya pamoja, kwa kuzingatia viwango vya kikanda na kimataifa.

6.6 Serikali na wadau wengine wanapaswa kuzingatia na kuchukua hatua za ziada kuyawezesha makundi yaliyo katika mazingira magumu ambayo kwa namna moja au nyingine hayawezi kufikia huduma za kiutawala na mahakama. Hatua hizi zinapaswa kujumuisha msaada wa kisheria, kama vile gharama nafuu, na zinaweza pia kujumuisha utoaji wa huduma ya wasaidizi-sheria au wapima-wasaidizi (sorovea) na huduma zinazohamishika kwa urahisi kwa jamii za vijijini na makundi ya watu asilia wanaohamahama.

6.7 Serikali zinapaswa kuhimiza taasisi za utekelezaji na mamlaka za mahakama kujenga utamaduni unaozingatia utoaji huduma bora na mwenendo wenye maadili. Taasisi na mamlaka za mahakama zinapaswa kupata mrejesho wa utoaji wa huduma mara kwa mara, kwa kufanya mahojiano na mtu mmoja mmoja na makundi yanayopata huduma, ili kuongeza viwango na kuboresha utoaji wa huduma, kukidhi matarajio, na kutimiza mahitaji mapya. Aidha, taasisi za utekelezaji na mamlaka za mahakama zinatakiwa kuweka wazi viwango vya ufanisi na kutoa taarifa ya matokeo mara kwa mara. Watumiaji wanapaswa kuwa na njia za kushughulikia malalamiko ndani ya taasisi za utekelezaji, kama vile kupitia muundo wa usimamizi, au nje ya taasisi, kama vile mapitio huru au kwa kumtumia mpokea malalamishi.

6.8 Taasisi zinazosimamia weledi wa taaluma zinazotoa huduma katika maeneo ya kumiliki zinapaswa kuandaa, kutangaza na kusimamia utekelezaji na utoaji huduma wa viwango vya juu vya mwenendo wa kimaadili. Wadau wa sekta za umma na zile za sekta binafsi wanapaswa kuzingatia viwango vya kimaadili vilivyowekwa na kuwajibishwa pale wanapovikiuka. Serikali haina budi kuandaa mazingira yanayofaa kuwezesha kuanzishwa kwa taasisi hizi pale ambapo hazipo.

6.9 Serikali na wadau wa mashirika yasiyo ya serikali wanapaswa kujitahidi kuzuia rushwa zinazohusiana na hakimiliki. Serikali zinapaswa kufanya hivyo hususani kupitia mashauriano na ushirikishwaji, utawala wa sheria, uwazi na uwajibikaji. Serikali zinapaswa kuandaa na kutekeleza hatua za kuzuia na kupambana na ufisadi zinazojumuisha udhibiti, matumizi ya nguvu kiholela kupita kiasi, kuzuia migogoro ya kimaslahi, na kutumia taratibu na kanuni zinazoeleweka. Aidha, Serikali zinapaswa kuweka mazingira wezeshi kwa minajili ya kurejelea uamuzi wa kiutawala na/au wa

kimahakama uliofanywa na taasisi za utekelezaji. Watumishi wanaofanya kazi za usimamizi wa umiliki wanapaswa kuwajibishwa kwa matendo yao. Aidha, watumishi wanapaswa kuwekewa mazingira ya kuwawezesha kutekeleza kazi zao kwa ufanisi. Vilevile, wanapaswa kulindwa dhidi ya kuingiliwa katika kutekeleza majukumu yao na uwezekano wa kulipiziwa kisasi kwa kutoa taarifa za matendo ya rushwa.

# Sehemu ya Tatu 3

## Utambuzi wa Kisheria na Ugawaji wa Hakimilki na Wajibu

Sehemu hii inahusu usimamizi wa miliki za ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu, kwa kuzingatia utambuzi wa kisheria kwa hakimiliki za watu asilia, wazawa, na jamii nyingine zenye mifumo ya kumiliki za kimila, hakimiliki zisizo rasmi; na ugawaji wa hakimiliki wa awali wa ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu inayomilikiwa au kusimamiwa na sekta ya umma.

### 7. Ulinzi wa hakimiliki

7.1 Katika jitihada za kutambua au kugawa haki za umiliki wa ardhi, maeneo ya uvuvi, na misitu, Serikali zinapaswa kuweka ulinzi, kwa mujibu wa sheria za nchi, ili kuepuka kuingilia au kusitisha hakimiliki za wengine, ikijumuisha hakimiliki halali ambazo kwa sasa hazina kinga ya sheria. Njia za kulinda hakimiliki hususani zinapaswa kuwalinda wanawake na wale walio katika mazingira magumu wanaomiliki hakimiliki zisizo na uhakika kama vile haki za nyongeza za ukusanyaji wa mazao.

7.2 Serikali zinapaswa kuhakikisha kwamba hatua zote zinazohusu utambuzi wa kisheria na ugawaji wa hakimiliki na wajibu wa umiliki yanaenda sawia na matakwa yaliyopo chini ya sheria za nchi na za kimataifa, na kwa kuzingatia matamko ya hiari ya nyenzo za kikanda na kimataifa.

7.3 Wakati ambapo Serikali zinakusudia kutambua au kugawa hakimiliki, zinapaswa kwanza kuainisha hakimiliki zote zilizopo na wamiliki wake, zilizoandikishwa na zisizoandikishwa. Watu asilia, wazawa, na jamii nyingine zenye mifumo ya miliki za kimila, wamiliki wadogo na yeyote ambaye anaweza kuathirika watapaswa kujumuishwa katika mchakato wa mashauriano sambamba na aya 3B.6 na 9.9. Serikali zinapaswa kuhakikisha upatikanaji wa haki, kwa mujibu wa aya ya 4.9, ikiwa watu wanaamini hakimiliki zao hazitambuliwi.

7.4 Serikali zinapaswa kuhakikisha kwamba wanawake na wanaume wanapata haki sawa katika hakimiliki mpya zilizotambuliwa, na kwamba haki hizo zimejumuishwa kwenye kumbukumbu za miliki. Pale inapowezekana, utambuzi wa kisheria na ugawaji wa hakimiliki za mtu mmojammoja, familia na jamii zinapaswa kufanyika kwa mpangilio, ukiendelea eneo kwa eneo kulingana na vipaumbele vya kitaifa. Hii itasaidia kuwapatia maskini na walio katika mazingira hatarishi fursa kamili za kupata utambuzi wa kisheria wa haki miliki zao. Msaada wa kisheria unapaswa kutolewa, hususani kwa maskini na watu walio katika mazingira hatarishi. Njia sahihi katika maeneo hayo zinapaswa kutumika ili kuongeza uwazi wakati kumbukumbu za haki miliki zinaandaliwa kwa mara ya kwanza, ikijumuisha utambuzi na uanishaji

wa hakimiliki.

7.5 Serikali zinapaswa kuhakikisha kwamba watu ambao hakimiliki zao zinatambuliwa au ambao wamepewa hakimiliki mpya wana uelewa wa kutosha wa haki zao na wajibu wao. Pale inapolazimu, Serikali zinapaswa kuweka mazingira kwa makundi hayo kufurahia hakimiliki zao na kutekeleza wajibu wao.

7.6 Pale ambapo haiwezekani kutoa utambuzi wa kisheria wa hakimiliki, Serikali zinapaswa kuzuia kuondolewa kwa lazima kusikoendana na matakwa yaliyopo chini ya sheria za kitaifa na za kimataifa na kwa mujibu wa kanuni za Miongozo hii.

## 8. Ardhi ya Umma, Maeneo ya Uvuvi na Misitu

8.1 Pale ambapo Serikali inamiliki au kudhibiti ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu, Serikali itawajibika kupanga matumizi na usimamizi wa maliasili kwa ajili ya mahitaji ya jamii, uchumi na mazingira kwa mapana. Aidha, Serikali zinapaswa kuhakikisha hatua zote za usimamizi zinawiana na majukumu ya sheria zilizopo za kitaifa na kimataifa na kuzingatia matamko ya hiari ya kikanda na kimataifa.

8.2 Pale ambapo Serikali inamiliki au kudhibiti ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu, hakimiliki za mtu mmoja mmoja na za makundi ya kijamii, ikijumuisha jamii zenye miliki za kimila hazina budi kutambuliwa, kuheshimiwa na kulindwa kwa uwiano na wajibu kwa mujibu wa sheria za nchi na za kimataifa kwa kuzingatia matamko ya hiari chini ya nyenzo za kikanda na kimataifa zinazotumika. Kwa mantiki hiyo, aina ya miliki halali zinapaswa kuainishwa kwa ufasaha na kuwekwa bayana kwa uwazi kwa mujibu wa sheria za nchi.

8.3 Kwa kutambua uwepo wa sehemu za ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu zilizoko chini ya umiliki wa umma na ambapo maeneo haya yanatumika na kusimamiwa na jamii kwa pamoja (kwa muktadha, katika mataifa mengine, maeneo haya yanajulikana kama ‘maeneo ya umma’), pale inapobidi, Serikali zinapaswa kutambua na kulinda maeneo ya ardhi, uvuvi na misitu yanayomilikwa na umma pamoja na mifumo jumuishi ya matumizi na usimamizi ikijumuisha michakato ya ugawaji wa unaofanywa na Serikali.

8.4 Serikali zinapaswa kuweka mifumo ya kumbukumbu za miliki za ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu zilizo chini ya miliki na udhibiti wake na kutunza daftari za wazi la kumbukumbu hizo. Daftari hizo zinapaswa kuweka kumbukumbu za wakala zinazohusika na usimamizi wa rasilimali na pia hakimiliki za watu asilia, wazawa, na makundi mengine ya jamii yenye hakimiliki za kimila na sekta binafsi. Pale inapowezekana Serikali zihakikishe hakimiliki za umma zinawekwa kwenye kumbukumbu pamoja na hakimiliki za watu asilia, wazawa, na makundi mengine ya jamii yenye hakimiliki za kimila na sekta binafsi kwenye mfumo mmoja wa kumbukumbu au zimeunganishwa katika mfumo wa ujumla.

8.5 Serikali zinapaswa kupambanua maeneo ya ardhi, uvuvi na misitu inayomiliki au kudhibiti yatakayokuwa chini ya uhifadhi na kutumiwa na sekta ya umma na yale yatakayotengwa kwa ajili ya matumizi ya watu wengine pamoja na masharti yake.

8.6 Serikali zinapaswa kutunga na kuweka bayana sera zinazohusu matumizi na usimamizi na udhibiti wa maeneo ya ardhi, uvuvi na misitu yanayomilikwa na sekta ya umma. Aidha, Serikali zinapaswa kutunga sera zitakazoimarisha mgawo wa faida zinazotokana na ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu kwa usawa. Sera hizo ni lazima zizingatie hakimiliki za watu wengine na mtu yeyote ambaye ataathiriwa na sera hizo anapaswa kujumuishwa katika mchakato wa majadiliano na ushirikishwaji sambamba na misingi ya majadiliano na ushiriki ya Miongozo hii. Usimamizi na miamala inayohusu maliasili inapaswa kufanyika kwa ufanisi, uwazi na uwajibikaji ili kukidhi sera za umma.

8.7 Serikali zinapaswa kutunga na kuweka bayana sera zinazohusu ugawaji hakimiliki kwa wengine na inapofaa kukasimisha wajibu wa usimamizi wa hakimiliki. Sera za ugawaji wa hakimiliki zinapaswa kuwa sambamba na malengo ya kijamii, kiuchumi na kimazingira kwa upana. Sera zinapaswa kuzingatia hakimiliki za wengine na mtu yeyote ambaye ataathiriwa na sera hizo anapaswa kujumuishwa katika mchakato wa majadiliano, ushirikishwaji na uamuzi. Sera hizo zihakikishe ugawaji wa hakimiliki hautishii maisha ya watu kwa kuwaondolea haki ya kuzifikia maliasili hizo.

8.8 Serikali zina mamlaka ya kugawa hakimiliki katika njia na mifumo mbalimbali, ikiwa ni pamoja na haki ya kutumia tu na hata kumiliki kabisa. Sera zinapaswa kutambua aina tofauti za hakimiliki na wamiliki wa haki hizo. Sera zinapaswa kuainisha mfumo wa ugawaji wa hakimiliki, kama vile ugawaji unaozingatia matumizi ya kihistoria au njia nyinginezo. Pale inapobidi watu waliopewa haki za miliki wanapaswa kuhakikishiwa uhuru wa kufaidi haki zao. Serikali zinapaswa kuweka bayana kama zinabakia na aina yoyote ya udhibiti kwenye maeneo ya ardhi, uvuvi na misitu yamegawiwa.

8.9 Serikali zinapaswa kugawa hakimiliki na kukasimisha usimamizi wa hakimiliki kwa uwazi, njia shirikishi, kwa kutumia taratibu rahisi zinazoeleweka na kufikiwa na watu wote, hususani, jamii asilia, wazawa, na jamii nyingine zinazofuata mifumo ya hakimiliki ya kimila. Taarifa zitolewe kwa washiriki wote kwa lugha zinazotumika, na kujumuisha ujumbe unaozingatia jinsia. Pale inapowezekana, Serikali zinapaswa kuhakikisha kuwa hakimiliki mpya zilizogawiwa zinaingizwa kwenye mfumo mmoja wa kumbukukumbu pamoja na hakimiliki zingine au zinaunganishwa kwenye mfumo wa jumla. Wadau wa kiserikali na wasio wa kiserikali wanapaswa kujitahidi kuzuia ufisadi katika ugawaji wa hakimiliki.

8.10 Kutegemea rasilimali zilizopo, Serikali zinapaswa kuhakikisha kwamba taasisi zinazohusika na ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu zinajitosheleza kwa kuwa na watumishi, miundombinu, fedha, na uwezo mwingine katika mifumo tofauti. Pale ambapo madaraka ya usimamizi wa hakimiliki

yamekasimishwa, wale waliokasimishwa wanapaswa kupewa mafunzo na kujengewa uwezo wa kutekeleza majukumu waliyopewa.

8.11 Serikali zinapaswa kufuatilia matokeo ya mipango ya ugawaji wa hakimiliki, ikijumuisha athari zilizotofautishwa kijinsia kwenye upatikanaji wa uhakika wa chakula na kutokomeza umaskini; pamoja na, athari zake kwenye malengo ya kijamii, kiuchumi na kimazingira, na kuanzisha jitihada za kurekebisha kama itakavyohitajika.

## 9. Jamii Asilia, Wazawa, na Jamii Nyingine Zenye Mifumo ya Umiliki wa Kimila

9.1 Serikali na wadau wasio wa kiserikali wanapaswa kutambua kwamba ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu ina thamani za kijamii, kiutamaduni, kiimani, kiuchumi, kimazingira na kisiasa kwa jamii asilia, wazawa, na jamii nyingine zenye mifumo ya umiliki wa kimila.

9.2 Jamii asilia, wazawa na watu wa jamii nyingine zenye mifumo ya umiliki wa kimila zinazosimamia ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu zinatakiwa kuimarisha na kutoa haki sawa, salama na endelevu kwenye maliasili hizo kwa kuzingatia umuhimu wa upatikanaji wa ardhi kwa wanawake. Ushirikishwaji sahihi wa watu wote, wanaume, wanawake na vijana katika kutoa uamuzi juu ya mifumo ya umiliki unapaswa kuimarishwa kupitia taasisi zilizopo katika jamii au za kitamaduni, pamoja na mifumo ya umiliki wa pamoja. Inapobidi, jamii zisaidiwe kuongeza uwezo wa wanajamii kushiriki kikamilifu katika utoaji wa uamuzi na usimamizi wa mifumo yao ya umiliki.

9.3 Serikali zinapaswa kuhakikisha kwamba shughuli zote zinazingatia matakwa yaliyopo kwa mujibu wa sheria za kitaifa na kimataifa, na kwa kuheshimu matamko ya hiari yaliyopo katika nyenzo za kikanda na kimataifa. Kwa upande wa jamii asilia na wazawa, Serikali zinapaswa kufikia matakwa au malengo na matamko yao ya hiari ili kulinda, kuimarisha na kutekeleza haki za binadamu kama zilivyo katika mkataba wa kimataifa wa Shirika la Kazi Duniani (Na.169) zinazohusu Jamii asilia na wazawa na Makabila katika Nchi Huru, Mkataba juu ya Uanuwai wa Kibaiolojia na wa Tamko la Umoja wa Mataifa juu ya Haki za watu wa Jamii asilia na wazawa

9.4 Serikali zinapaswa kuweka utambuzi sahihi na ulinzi wa hakimiliki halali za jamii asilia, wazawa na jamii nyingine zenye mifumo ya umiliki wa kimila inayoambatana na matakwa yaliyopo chini ya sheria za kitaifa na kimataifa, na kwa kuzingatia matamko ya hiari yaliyopo katika nyenzo za kikanda na kimataifa. Utambuzi huo unapaswa kuzingatia maeneo ya ardhi, uvuvi na

misitu yanayotumiwa na jamii pekee na yale yanayotumika kwa pamoja na uheshimu kanuni za usimamizi wenye uwajibikaji. Taarifa juu ya utambuliwaji zinapaswa kuenezwa katika maeneo yanayofikika, kupitia mfumo unaoeleweka na kwa lugha nyepesi.

9.5 Pale jamii asilia, wazawa na jamii nyingine zenye mifumo ya umiliki wa kimila wana hakimiliki halali kwenye maeneo ya urithi wanapoishi, Serikali zinapaswa kutambua na kulinda haki hizi. Jamii asilia, wazawa na jamii nyingine zenye mifumo ya umiliki wa kimila hawapaswi kuondolewa kwa nguvu kutoka katika maeneo hayo ya urithi.

9.6 Serikali zinapaswa kutumia sera, sheria na mifumo ya kiutawala kutambua mifumo ya umiliki wa jamii asilia, wazawa na jamii nyingine zenye mifumo ya umiliki wa kimila. Endapo mabadiliko ya kisera au kisheria yanaimarisha haki za wanawake lakini ikawaweka katika migogoro na kiutamaduni, wadau wote wanapaswa kushirikiana kuhusisha mabadiliko hayo katika mifumo ya miliki za kimila.

9.7 Katika kuandaa sera na sheria zinazohusu miliki, Serikali zinapaswa kuzingatia maadili ya kijamii, kitamaduni, kiimani, kiuchumi na kimazingira juu ya ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu iliyopo kwenye mifumo ya jamii asilia, wazawa na jamii nyingine zenye mifumo ya umiliki wa kimila. Ushirikishwaji kamili na makini wa watu wote au wawakilishi wa jamii zilizoathirika, ikiwa ni pamoja na watu walio katika mazingira magumu na waliokandamizwa, unapaswa kuzingatiwa wakati wa kutayarisha sera na sheria zinazohusu mifumo ya umiliki ya jamii asilia, wazawa na jamii nyingine zenye mifumo ya umiliki wa kimila.

9.8 Serikali zinapaswa kulinda jamii asilia, wazawa na jamii nyingine zenye mifumo ya umiliki wa kimila dhidi ya matumizi yasiyoruhusiwa ya ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu kutumiwa na watu wengine. Pale ambapo jamii haiwezi kupinga, Serikali zinapaswa kusaidia kuweka kumbukumbu rasmi na kueneza taarifa za asili na mahali ambapo maeneo ya ardhi, uvuvi na misitu yalipo na namna yanavyotumiwa na kusimamiwa na jamii. Vilevile, pale ambapo kumbukumbu za hakimiliki za wazawa, jamii asilia na jamii nyingine zenye mifumo ya umiliki wa kimila zimewekwa rasmi, kumbukumbu hizo zinapaswa kujumuisha haki miliki za umma mwingine, miliki binafsi na miliki za pamoja ili kuzuia madai yanayokinzana.

9.9 Serikali na wadau wengine wanapaswa kushauriana na wazawa na jamii asilia kabla ya kuanzisha mradi wowote au kutekeleza hatua za kisheria au kiutawala zitakazoathiri maliasili ambapo jamii hizo zina haki. Miradi hiyo

inapaswa kujengwa juu ya misingi ya ushirikishaji wa jamii asilia na wazawa kupitia asasi zinazoiwakilisha jamii ili kupata kibali chao cha awali, huru na kitokanacho na taarifa kutoka kwa wazawa na jamii asilia kwa mujibu wa Tamko la Umoja wa Mataifa la Haki za Jamii Asilia na Wazawa na kwa kuzingatia nafasi na uelewa wa kila Serikali. Michakato ya ushauri na maamuzi inapaswa kutambuliwa bila kuingiliwa au kubughudhiwa na ifanyike katika mazingira ya kuaminika. Vile vile, misingi ya utoaji wa ushauri na ushirikishwaji ya watu wa jamii asilia na Wazawa, kama ilivyoainishwa katika aya ya 3B.6 na katika sehemu hii, inapaswa kutumika.

9.10 Serikali na wadau wasio wa kiserikali, asasi zinazowakilisha jamii zilizoathirika na kwa ushirikiana na jamii zilizoathirika wanapaswa kujitahidi kutoa msaada wa kitaalamu na kisheria kwa jamii na kushiriki katika uandaaji wa sera, sheria na miradi katika hali isiyo ya kibaguzi na inayozingatia uwakilishi wa jinsia.

9.11 Serikali zinapaswa kuheshimu na kuimarisha njia zinazotumiwa na jamii asilia na Wazawa na zingine zenye mifumo ya umiliki wa kimila katika utatuzi wa migogoro ndani ya jamii hizoinayoambatana na na matakwa yaliyopo chini ya sheria za kitaifa na kimataifa na kwa kuzingatia matamko ya hiari yaliyopo kwenye nyenzo za kikanda na kimataifa. Kwa upande wa maeneo ya ardhi, uvuvi na misitu yanayotumiwa na jamii zaidi ya moja, njia za utatuzi wa migogoro baina ya jamii zinapaswa kuimarishwa au kuanzishwa.

9.12 Serikali na wadau wasio wa kiserikali wanapaswa kujaribu kuzuia ufisadi katika mifumo ya umiliki ya jamii asilia, wazawa na watu wa jamii nyingine zenye mifumo ya umiliki wa kimila kwa kushauriana na kuishirikisha jamii, pia kwa kuzijengea uwezo jamii hizo.

## 10. Umiliki Usiorasmi

10.1 Pale ambapo kuna umiliki wa ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu usiorasmi, Serikali zinapaswa kuutambua na kuuheshimu kama ilivyo kwenye hakimiliki rasmi zilizopo kwa mujibu wa sheria za nchi; na kwa njia zinazotambua uhalisi na kuimarisha ustawi wa kijamii, kiuchumi na kimazingira. Vile vile, Serikali zinapaswa kuimarisha sera na sheria ili kutambua umiliki usio rasmi. Mchakato wa uundaji wa sera na sheria hizo unapaswa kuwa shirikishi, unaozingatia jinsia na unaojitahidi kutoa msaada wa kiutaalamu na kisheria kwa jamii zilizoathirika na kwa mtu mmojammoja. Kwa namna ya pekee, Serikali zinapaswa kutambua kuwapo kwa uibukaji wa umiliki usiorasmi unaotokana na wahamiaji wakubwa.

10.2 Serikali zinapaswa kuhakikisha kuwa shughuli zote zinazohusu umiliki usio rasmi, ikiwa ni pamoja na haki ya makazi yanayotosheleza, zinaendana na matakwa ya kisheria ya kitaifa na kimataifa yaliyopo na kwa kuzingatia matamko ya hiari yaliyopo kwenye nyenzo za kikanda na kimataifa.

10.3 Popote Serikali zinapotambua kisheria umiliki usio rasmi, utambuaji huu ufanyike kwa njia ya ushirikishwaji, kwa michakato inayojali jinsia na kwa kuzingatia haki za wapangaji. Katika kufanya hivyo, Serikali zinapaswa kuwaangalia kwa umakini wakulima na wazalishaji wadogowadogo wa chakula.  Michakato hii inapaswa kuwezeshwa ufikiwaji wa huduma kirahisi na kupunguza gharama. Pia, Serikali zinapaswa kujitahidi kutoa msaada wa kitaalamu na kisheria kwa jamii na wahusika wengine katika michakato hiyo.

10.4 Serikali zinapaswa kuchukua hatua zote stahiki ili kuzuia umiliki usio rasmi unaotokana na matakwa magumu ya kisheria na kiutawala juu ya mabadiliko ya matumizi na uendelezaji wa ardhi. Mahitaji na michakato ya uendelezaji wa ardhi iwe wazi, rahisi na ya gharama nafuu ili kupunguza wajibu wa kutekeleza

10.5 Serikali zinapaswa kujitahidi kuzuia rushwa, hususani kwa kuongeza kiwango cha uwazi, kwa kuwawajibisha watoa uamuzi na kwa kuhakikisha kwamba uamuzi usiotegemea au kuegemea upande wowote unatolewa kwa haraka.

10.6 Wakati inaposhindikana kutoa utambuzi wa kisheria juu ya umiliki usio rasmi, Serikali zinapaswa kuzuia uondoaji watu kwa nguvu zinazokiuka viwango vya sheria za kitaifa na kimataifa vilivyoko na kwa kuzingatia matamkoyaliyoko katika sehemu ya 16.

# Sehemu ya Nne 4

## Uhamisho na Mabadiliko Mengine ya Hakimiliki na Wajibu

Sehemu hii inahusu usimamizi wa hakimiliki ya ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu pale ambapo haki zilizopo, na wajibu unaoendana nazo, huhamishwa au kugawiwa upya kwa njia za hiari au za lazima kupitia masoko, miamala katika hakimiliki kutokana na uwekezaji, uunganishaji ardhi na mbinu nyingine za maboresho, fidia, ugawaji au utaifishaji ardhi.

### 11. Masoko

11.1 Pale inapofaa, serikali zitambue na kusimamia masoko ya mauzo na mikataba ya upangishaji kama njia ya kuhamisha haki ya matumizi na umiliki wa ardhi, maeneo ya uvuvi, na misitu. Pale ambapo mifumo ya masoko katika hakimiliki inafanya kazi, serikali zihakikishe kwamba shughuli zote zinaendana na majukumu yaliyopo chini ya sheria za kitaifa na kimataifa, na kwa kuzingatia ahadi za hiari chini ya nyenzo za kitaifa na kimataifa. Miamala ya hakimiliki kwenye ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu ifuate kanuni za Taifa za udhibiti wa matumizi ya ardhi na zisihatarishe malengo ya msingi ya maendeleo.

11.2 Serikali zinapaswa kuwezesha uendeshaji wa masoko kwa ufanisi na uwazi ili kuhamasisha ushiriki katika hali ya usawa na fursa sawa kwa ajili ya uhamisho wa hakimiliki wenye manufaa ili kupunguza migogoro na misukosuko; kuendeleza matumizi endelevu ya ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu na uhifadhi wa mazingira; kuhamasisha haki sawa na linganifu za matumizi ya rasilimali za ukoo zinazohusiana na ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu kulingana na mikataba inayohusika; kutanua fursa za kiuchumi, na kuongeza ushiriki wa watu maskini. Serikali zichukue hatua kuzuia madhara yasiyotakiwa katika jamii hizo, jamii asilia, wazawa na makundi yaliyo katika mazingira hatarishi ambayo yanaweza kujitokeza, pamoja na mambo mengine, ulanguzi wa ardhi, ulimbikizaji wa ardhi na matumizi mabaya ya hakimiliki za kimila. Serikali na wadau wengine watambue kwamba maadili, kama ya kijamii, kiutamaduni na kimazingira, si mara zote yanahudumiwa ndani ya masoko yasiyodhibitiwa. Serikali zilinde masilahi mapana ya jamii kupitia sera na sheria zinazofaa za hakimiliki.

11.3 Serikali zinapaswa kutunga sera na sheria na kuanzisha mifumo ya udhibiti na wakala ili kuhakikisha shughuli za soko zenye uwazi na ufanisi,

kuruhusu upatikanaji usio na ubaguzi, na kuzuia njia zenye ushindani. Serikali zinapaswa kurahisisha taratibu za utawala ili kuepusha kukatisha tamaa ya ushiriki katika masoko kwa watu maskini na walio zaidi katika mazingira hatarishi.

11.4 Serikali na wadau wengine wanapaswa kuhakikisha kuwa taarifa za miamala sokoni na taarifa juu ya thamani za masoko zipo wazi na zinasambazwa kwa upana, kwa kuzingatia vizuizi vya usiri binafsi. Serikali zisimamie taarifa hizi na kuchukua hatua pale masoko yanapokuwa na matokeo yasiyofaa au kutokuhamasisha ushiriki wa soko kwa upana na usawa.

11.5 Serikali zianzishe mifumo inayofaa na kuaminika ya utunzaji kumbukumbu, kama vile masijala ya ardhi, inayotoa upatikanaji wa taarifa za hakimiliki na wajibu ili kuongeza usalama wa miliki na kupunguza gharama na kuepusha hatari ya miamala.

11.6 Serikali zianzishe ulinzi ili kulinda hakimiliki halali za wanandoa, wanafamilia na wengine wasiooneshwa kama wana haki kwenye hakimiliki zilizoingizwa katika mifumo ya kutunza kumbukumbu, kama vile masijala ya ardhi.

11.7 Wahusika wa serikali na wasiokuwa wa serikali wanapaswa kuzingatia viwango vya maadili vitumikavyo. Wanapaswa kueneza na kufuatilia utekelezaji wa viwango hivi katika uendeshaji wa masoko ili kuzuia rushwa, hasa kwa kuweka wazi kwa umma.

11.8 Kwa kuzingatia umuhimu wa wazalishaji wadogo kwa uhakika wa chakula na ustawi wa jamii wa taifa, Serikali zihakikishe kwamba zinaposimamia shughuli za masoko za miamala ya miliki, zinalinda haki miliki za wazalishaji wadogo.

## 12. Uwekezaji

12.1 Serikali na watendaji wasio wa serikali watambue kwamba uwekezaji wa umma na binafsi ni wa muhimu katika kuboresha usalama wa chakula. Utawala wenye uwajibikaji wa hakimiliki ya ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu unahamasisha wamiliki wa hakimiliki kufanya uwekezaji wenye uwajibikaji katika maliasili hizi, na kuongeza uzalishaji endelevu wa mazao ya kilimo na kuzalisha kipato kikubwa zaidi. Serikali zihamasishe na kusaidia uwekezaji wenye uwajibikaji katika ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu unaochangia katika malengo makubwa ya kijamii, kiuchumi, na kimazingira chini ya mifumo mbalimbali ya kilimo. Serikali zihakikishe

kwamba, matendo yote yanalingana na majukumu yaliyopo chini ya sheria za kikanda na kimataifa.

12.2 Kwa kuzingatia kwamba wazalishaji wadogo na vyama vyao katika nchi zinazoendelea wanatoa mchango mkubwa katika uwekezaji wa kilimo wenye mchango muhimu katika uhakika wa chakula, lishe, kuondoa umaskini na kurudisha ardhi katika hali ya awali, Serikali ziunge mkono uwekezaji wa wawekezaji wadogo, na vilevile uwekezaji wa umma na binafsi inaozingatia mahitaji maalumu ya wawekezaji wadogo.

12.3 Aina zote za miamala katika hakimiliki kama matokeo ya uwekezaji katika ardhi, uvuvi na misitu zifanyike kwa uwazi kwa kuzingatia sera za kitaifa za sekta zinazohusika na ziendane na malengo ya kukua kijamii na kiuchumi na maendeleo endelevu ya binadamu yaliyojikita zaidi kwa wakulima wadogo.

12.4 Uwekezaji makini usilete madhara yoyote, bali ufanikishe ulinzi dhidi ya kutoweka kwa hakimiliki halali na uharibifu wa mazingira, na uheshimu haki za binadamu. Uwekezaji huu ufanywe kwa ubia na kupitia ngazi mbalimbali za serikali na kushirikisha na kuheshimu haki halali za umiliki za jamii asilia na wazawa.Wajitahidi kuendelea kuchangia katika malengo ya sera, kama vile kuondoa umaskini; kufanikisha upatikanaji wa chakula na matumizi endelevu ya ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu, kusaidia jamii, kuchangia katika maendeleo ya kijiji, kukuza na kulinda mifumo ya kijamii ya uzalishaji wa chakula katika jamii; kuboresha maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi; kuanzisha ajira; kutofautisha shughuli za uingizaji kipato; kuleta faida kwa nchi na watu wake, wakiwamo maskini na walio kwenye mazingira hatarishi zaidi; na kwa kufuata sheria za viwango vya msingi vya kazi za kitaifa na kimataifa; vilevile, kutumika inavyofaa, kanuni zinazoendana na viwango vya Shirika la Kazi Duniani.

12.5 Serikali, kwa mashauriano na ushirikiano unaofaa, zitoe kanuni za wazi, juu ya kipimo, uwezo na asili ya miamala katika hakimiliki zilizoruhusiwa na ifafanue nini kinahusisha kipimo cha miamala mikubwa katika hakimiliki katika muktadha wao wa kitaifa.

12.6 Serikali zitoe ulinzi kwa kulinda hakimiliki halali, haki za binadamu, shughuli za watu zenye kuwaingizia kipato, uhakika wa chakula na mazingira kutoka kwenye hatari inayoweza kujitokeza kwenye miamala mikubwa ya hakimiliki. Ulinzi huo unaweza kuhusisha kuweka kikomo cha juu cha bei kwa miamala ya ardhi iliyoruhusiwa na kudhibiti namna ambavyo uhamisho utakaozidi kiwango fulani utaidhinishwa, kama vile

kwa idhini ya Bunge. Serikali zifikirie kuhamasisha uzalishaji mbalimbali na mtindo wa uwekezaji ambao hautasababisha kutokea kwa uhamisho mkubwa wa hakimiliki kwenda kwa wawekezaji, na uhamasishe ubia na wamiliki wa hakimiliki ambao ni wenyeji.

12.7 Kwa upande wa jamii asilia, wazawa na jamii zao, Serikali zihakikishe kwamba matendo yote yanaendana na majukumu yaliyopo chini ya sheria za kitaifa na kimataifa, na kwa kuzingatia ahadi za hiari zilizopo katika nyenzo za kitaifa na kimataifa, pamoja na, kama ifaavyo, Makubaliano ya Shirika la Kazi Duniani (Namba 169) kuhusu jamii asilia, wazawa na watu waliotengwa na Azimio la Umoja wa Mataifa juu ya Haki za Jamii asilia na Wazawa. Serikali na wadau wengine wafanye mashauri ya uaminifu na jamii asilia na wazawa kabla ya kuanzisha mradi wowote wa uwekezaji ambao utaathiri rasilimali ambazo jamii zina hakimiliki. Miradi hiyo ijikite kwenye mashauri yenye tija na maana ya wanachama wa jamii asilia na wazawa kama ilivyoelezwa katika sehemu ya 9.9. Kanuni za mashauri na ushirikishaji za Mwongozo huu zitumike kwa uwekezaji ambao unatumia rasilimali za jamii zingine.

12.8 Serikali ziamue pamoja na wote walioathirika, kulingana na kanuni za mashauri na ushirikishwaji za Mwongozo huu, mazingira ambayo yanahamasisha uwekezaji wenye uwajibikaji na kisha iendeleze na kutangaza sera na sheria zinazohamasisha uwekezaji wenye uwajibikaji, kuheshimu haki za binadamu, na kuhamasisha uhakika wa chakula na matumizi endelevu ya ardhi. Sheria ziagize kwamba makubaliano ya uwekezaji yafafanue kwa uwazi haki na wajibu wa kila mmoja aliyepo kwenye makubaliano. Makubaliano ya uwekezaji yafuate mfumo wa kitaifa wa sheria na kanuni za uwekezaji.

12.9 Serikali zifanye mipango ya uwekezaji inayojumuisha aina zote za miamala ya hakimiliki, ikiwamo makubaliano ya utwaaji ardhi na ubia, kulingana na kanuni za mashauri na ushiriki wa Mwongozo huu, na wale ambao hakimiliki zao, zikiwamo haki ndogo, wanaweza kuathirika. Serikali na pande zingine zinazohusika, ziwafahamishe watu, familia na jamii juu ya hakimiliki zao, na kuwasaidia kuendeleza uwezo katika kufanya mashauri na ushiriki, ikiwamo kutoa msaada wa kitaalamu kadri inapohitajika.

12.10 Pale ambapo uwekezaji unahusisha miamala mikubwa ya hakimiliki, ikiwamo makubaliano ya utwaaji na ubia, yanafikiriwa, serikali zijitahidi kuweka vifungu vya kutaka pande mbalimbali kufanya tathmini juu ya matokeo hasi na chanya ambayo uwekezaji unaweza kuyaleta juu ya

hakimiliki, uhakika wa chakula na ufahamu endelevu juu ya haki ya chakula cha kutosha, shughuli za kuingiza kipato na mazingira. Serikali zihakikishe kwamba haki halali zilizopo za miliki na madai, ikiwemo ile ya kitamaduni na hakimiliki zisizo rasmi, zinatambuliwa kwa mfumo maalumu na wa haki, pia na haki na shughuli za kujiingizia kipato za watu wengine ambao pia wameathiriwa na uwekezaji, kama vile, wazalishaji wadogo. Mchakato huu unapaswa kufanyika kupitia mashauriano na pande zote zilizoathirika kulingana na kanuni za mashauriano na ushirikishwaji za mwongozo huu. Serikali zinapaswa kuhakikisha kwamba haki zilizopo za hakimiliki haziathiriwi na uwekezaji huo.

12.11 Pande zote zinazoingia katika makubaliano zitoe taarifa za kujitosheleza kuhakikisha kwamba watu wote wanahusika na kupewa taarifa katika majadiliano, na waombe kwamba makubaliano yanahifadhiwa kwa maandishi na yanaeleweka na wote waliothirika. Utaratibu wa majadiliano uwe ule usiobagua na uzingatie jinsia.

12.12 Wawekezaji wana wajibu wa kuheshimu sheria za kitaifa na zilizotungwa na kutambua na kuheshimu hakimiliki za watu wengine na utawala wa sheria unaozingatia kanuni za jumla kwa watendaji wa asasi zisizo za serikali kama ilivyo katika Mwongozo huu. Uwekezaji usichangie katika ukosefu wa chakula na uharibifu wa mazingira.

12.13 Wataalamu wanaotoa huduma serikalini, wawekezaji na wamiliki wa hakimiliki za ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu wafanye bidii kwa kadiri ya uwezo wao, wakati wa kutoa huduma, bila kujali kwamba huduma hiyo inaombwa kufanyika.

12.14 Serikali na waliothirika wachangie katika ufuatiliaji madhubuti wa utekelezaji na athari za makubaliano yanayohusisha mabadilishano makubwa ya kibiashara ya hakimiliki, ikiwamo makubaliano ya mapato na ubia. Serikali irekebishe inapobidi kutekeleza makubaliano na kulinda hakimiliki na haki zingine na kuweka utaratibu ambapo pande zilizodhulumiwa zinaweza kuomba zoezi hilo.

12.15 Serikali zinapowekeza au kuhamasisha uwekezaji nje ya nchi, zihakikishe kwamba kitendo hicho kinaendana na kulinda hakimiliki halali, uimarishaji wa usalama wa chakula na majukumu yaliyopo chini ya sheria za kitaifa na kimataifa, na kwa kuzingatia ahadi za hiari zilizopo katika nyenzo za kitaifa na kimataifa.

## 13. Kuunganisha Vipande vya Ardhi na Njia Zingine za Marekebisho

13.1 Kadri inavyofaa, Serikali inaweza ikafikiria uwezekano wa kuunganisha vipande vya ardhi, kubadilishana au njia zingine za hiari za marekebisho ya vipande vya ardhi au mashamba ili kuwasaidia wamiliki na watumiaji ardhi kuboresha mpangilio na matumizi ya ardhi yao au mashamba ikiwamo kuimarisha uhakika wa upatikanaji chakula na maendeleo ya vijijini kwa namna endelevu. Serikali zihakikishe kwamba hatua zote hizi zinalingana na majukumu yake chini ya sheria za kitaifa na kimataifa na kwa kuzingatia ahadi za hiari kupitia nyenzo mbali mbali za kikanda na kimataifa, na kuhakikisha kuwa angalau hali ya maisha ya washiriki inakuwa ikilinganishwa na hali kabla ya mradi. Utaratibu huu utumike kuratibu mapendeleo ya wamiliki wengi na watumiaji katika mradi mmoja wa marekebisho uliohalalishwa.

13.2 Pale itakapofaa, Serikali zinaweza kufikiria kuanzisha hifadhi ya ardhi kama sehemu ya mradi wa kuunganisha vipande vya ardhi kwa kutwaa na kuhodhi ardhi kwa muda mfupi mpaka itakapogawiwa kwa wanufaika wa mradi.

13.3 Pale itakapofaa, serikali zifikirie, kuhamasisha na kuwezesha uunganishaji wa vipande vya ardhi na kutenga hifadhi ya ardhi kwa ajili ya kulinda mazingira na miradi ya miundombinu. Hatua hii itawezesha utwaaji wa ardhi inayomilikiwa na watu binafsi kwa ajili ya miradi ya umma na kuwasaidia wananchi wanaomiliki ardhi, wakulima wakubwa na wadogo watakaoathirika, kulipwa fidia itakayowawezesha kuendelea na hata kuongeza uzalishaji katika shughuli zao.

13.4 Pale ambapo mashamba na maeneo ya misitu ya familia za wakulima wadogo yamegawanywa katika vipande vidogo vidogo na hivyo kusababisha gharama za uzalishaji kuongezeka, Serikali zinaweza kufikiria kuunganisha vipande vya ardhi na kuanzisha hifadhi za ardhi ili kuboresha muundo wa mashamba hayo na misitu. Hata hivyo, pale ambapo mgawanyiko wa mashamba na misitu katika vipande vidogovidogo una manufaa, kama vile kupunguza hatari mbalimbali au kilimo cha mazao mseto, Serikali ziepuke kutumia mbinu ya kuhuisha ukubwa wa ardhi na kuanzisha hifadhi za ardhi. Miradi ya kuunganisha vipande vya ardhi na kubadilisha muundo wa mashamba inapaswa kujumuishwa katika miradi ya kuwawezesha wakulima kama vile ukarabati wa mifumo ya umwagiliaji na barabara za eneo hilo. Aidha, Serikali ziandae hatua za kulinda uwekezaji unaofanyika katika kuunganisha vipande vya ardhi kwa kuzuia ukataji wa vipande vidogovidogo vya ardhi iliyounganishwa.

13.5 Serikali zianzishe mikakati ya mbinu za upangaji upya wa ardhi unaoambatana na mahitaji ya eneo linalohusika. Mikakati hiyo iwe endelevu kijamii, kiuchumi na kimazingira, na izingatie jinsia. Aidha, mikakati hiyo iainishe kanuni na malengo ya upangaji upya, wanufaikaji, na kujenga uwezo na ujuzi katika sekta za umma na binafsi, vikundi vya wakulima na wazalishaji wadogo, wavuvi, watumiaji misitu, na wanazuoni. Sheria zianzishe taratibu zinazoeleweka na za gharama nafuu kwa ajili ya kusimamia upangaji wa maeneo au mashamba madogo na matumizi yake.

13.6 Serikali zianzishe mikakati inayofaa katika miradi, kwa kutumia mbinu za upangaji upya wa ardhi. Serikali zina jukumu la kuwasiliana na kuwapa taarifa za kutosha na katika lugha wanazotumia wale wote wanaoweza kuathirika na mradi kama vile mtu binafsi, kikundi cha watu au jamii. Aidha, waathirika wanapaswa kupewa msaada wa kitaalamu na kisheria. Mbinu shirikishi na zinazozingatia jinsia zitumike kwa kuzingatia haki za jamii asilia na wazawa. Ulinzi wa mazingira uanzishwe kuzuia au kupunguza uharibifu na upotevu wa viumbehai na kuleta mabadiliko ambayo yatahamasisha usimamizi bora wa ardhi, utendaji bora na urudishaji ardhi katika hali nzuri.

## 14 Urejeshaji wa Hakimiliki

14.1 Pale itakapofaa, kwa kuzingatia muktadha wa kitaifa, Serikali ziangalie uwezekano wa kuwarejeshea wale wote walioathirika, hakimiliki halali zilizopotea za ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu.Serikali zihakikishe kwamba urejeshaji huo unalingana na majukumu yao chini ya sheria za kitaifa na kimataifa, kwa kuzingatia ahadi za hiari kwa mujibu wa nyenzo zinazohusika za kikanda na kimataifa.

14.2 Pale itakapowezekana, vipande vya ardhi vilivyochukuliwa virejeshwe kwa wale waliopoteza au warithi wao, kwa uamuzi wa mamlaka za kitaifa. Pale ambapo vipande vya ardhi vilivyotwaliwa haviwezi kurejeshwa kwa wamiliki wa awali, serikali itoe fidia kwa wakati na yenye kuzingatia usawa. Fidia hii iwe katika mfumo wa fedha na/au ardhi au shamba dogo mbadala, ikizingatiwa na kuhakikisha kuwa waathirika wote wanahudumiwa kwa usawa.

14.3 Pale itakapofaa, masuala ya urejeshaji wa ardhi inayomilikiwa na jamii asilia na wazawa yashughulikiwe katika muktadha wa kitaifa kwa mujibu wa katiba ya kitaifa na sheria..

14.4 Serikali ianzishe sera na sheria ambazo zitaruhusu taratibu za wazi na zinazoeleweka za urejeshaji hakimiliki. Taarifa juu ya taratibu za urejeshwaji hakimiliki zisambazwe kwa kiasi kikubwa katika lugha inayotumika. Wadai wapewe msaada wa kutosha, ikiwamo msaada wa kisheria wakati wote wa mchakato. Serikali zihakikishe kwamba madai ya urejeshaji yanashughulikiwa kwa haraka na kwa wakati. Inapobidi, wadai waliofanikiwa wapewe huduma zitakazowawezesha kufurahia hakimiliki zao na kutekeleza majukumu yao. Maendeleo ya utekelezwaji wa urejeshaji yatangazwe kwa umma kwa mapana.

## 15. Mabadiliko ya Ugawaji

15.1 Mabadiliko ya ugawaji huwezesha upatikanaji wa ardhi kwa kiwango kikubwa, kwa usawa na katika maendeleo ya maeneo ya vijijini. Katika hali hii, Serikali zinaweza kuweka njia za utoaji wa ardhi ya umma, za hiari na zinazoendana na hali ya soko ikiwa ni pamoja na utwaaji wa ardhi binafsi, maeneo ya uvuvi na misitu pale inapofaa.

15.2 Serikali zinapaswa kuzingatia viwango vya juu vya ardhi kuwa suala la kisera katika muktadha wa utekelezaji wa mabadiliko ya ugawaji.

15.3 Katika muktadha wa kitaifa na kwa mujibu wa sheria na kanuni za kitaifa, mabadiliko ya ugawaji yanaweza kufikiriwa kwa sababu za kijamii, kiuchumi, kimazingira, na kadhalika ambapo kiwango kikubwa cha umiliki kinafungamana na hali ya juu ya umaskini katika maeneo ya vijijini na kinachangia kukosekana kwa upatikanaji wa ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu kufungamana na vifungu katika sehemu ya 15 inayohusu haki za wamiliki wote halali. Mabadiliko ya ugawaji yanapaswa kuwahakikishia wanaume na wanawake upatikanaji wa ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu kwa usawa.

15.4 Pale Serikali zinapochagua kutekeleza mabadiliko ya ugawaji, zinapaswa kuhakikisha kwamba mabadiliko yanaendana na majukumu ya Serikali hizo, sheria za kitaifa na kimataifa, na ahadi za hiari katika nyenzo za kikanda na kimataifa. Mabadiliko yanapaswa kufuata utawala wa sheria na yatekelezwe kwa mujibu wa sheria na taratibu za kitaifa. Serikali zinapaswa kuwezesha ongezeko la mashauriano yanaendana na misingi ya Miongozo hii juu ya ugawaji, ikiwa ni pamoja na kuweka uwiano sahihi wa mahitaji ya wadau wote na juu ya njia zitakazotumika. Ushirika kati ya Serikali; jamii; asasi za kiraia; sekta binafsi; makundi ya wakulima na ya wazalishaji wadogo wa chakula, wavuvi na watumiaji wa misitu na wadau wengine unapaswa kuanzishwa. Michango ya kifedha na mingineyo inayotarajiwa na wanufaikaji inapaswa kuwa ya kutosha na isiyowaachia

mizigo ya madeni wasiyomudu. Wale wanaotoa hakimiliki zao kwenye ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu wanapaswa kupata malipo stahiki bila ucheleweshaji.

15.5 Pale Serikali zinapochagua kutekeleza mabadiliko ya ugawaji, malengo ya miradi ya mabadiliko yanapaswa kufafanuliwa na ardhi isiyohusishwa na ugawaji inapaswa kuainishwa. Wanufaikaji wanaolengwa, kama vile familia pamoja na wale wanaotafuta maeneo ya makazi, wanawake, wakazi wasio rasmi, wafugaji, makundi yaliyokandamizwa kwa muda mrefu, makundi yaliyotengwa, vijana, watu wa jamii asilia, wazawa, wawindaji-wakusanyaji ndani ya misitu na wazalishaji wadogo wa chakula wanapaswa kuainishwa kwa uwazi.

15.6 Pale Serikali zinapochagua kutekeleza mabadiliko ya ugawaji, zinapaswa kutunga sera na sheria kupitia michakato ya ushirikishaji ili kuvifanya vyombo hivi endelevu. Serikali zinapaswa kuhakikisha kwamba sera na sheria zinawasaidia wanufaikaji, iwe ni jamii au mtu mmoja mmoja, kujifunza kiwango cha wastani cha maisha ambacho ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu vinahitaji. Vilevile, Serikali zinapaswa kuhakikisha kuwa wanaume na wanawake wanafikiriwa kwa usawa katika mabadiliko ya ugawaji. Serikali zinapaswa kurekebisha sera ambazo zinaweza kuzuia ufikiwaji kwa uendelevu matarajio yaliyokusudiwa ya mabadiliko ya ugawaji.

15.7 Pale mabadiliko ya ugawaji yanapozingatiwa, Serikali zinaweza kutathmini athari chanya na hasi zinazoweza kutokea baada ya mabadiliko ya ugawaji zinazohusu hakimiliki, uhakika wa chakula na ufikiwaji wa haki ya chakula kinachotosheleza, riziki, na mazingira. Mchakato wa tathmini unapaswa kufanyika kwa mujibu wa misingi ya mashauri na ushirikishaji wa Miongozo hii. Tathmini zinaweza kutumika kama misingi ya kutambua njia zinazohitajika kuwasaidia wanufaikaji na kuboresha miradi ya ugawaji.

15.8 Serikali zinapaswa kuhakikisha kwamba miradi ya ugawaji wa ardhi inaeleza kiwango kamili cha msaada unaohitajiwa na wanufaikaji. Msaada huu unaweza kuwa upatikanaji wa mikopo, bima za mazao, pembejeo, masoko, msaada wa kitaalamu wa ugavi vijijini, uendelezaji wa mashamba na nyumba. Utoaji wa msaada wa huduma unapaswa kufungamanishwa na mabadiliko juu ya ardhi yanayofanywa na wanufaikaji. Gharama kamili za mabadiliko ya ardhi, ikiwa ni pamoja na gharama za huduma saidizi, zinapaswa kutambuliwa mapema na kujumuishwa katika bajeti.

15.9 Serikali zinapaswa kutekeleza mabadiliko ya ugawaji kwa njia za wazi, shirikishi na taratibu za uwajibikaji. Wadau wote walioathirika wanapaswa kupitishwa katika mchakato mahususi na kupewa fidia ya haki kwa mujibu wa sheria za kitaifa na vifungu vilivyoainishwa katika sehemu ya 16. Waathirika wote, wakijumuisha makundi yaliyokandamizwa, wanapaswa kupokea taarifa kamili na za wazi zinazojumuisha taarifa za makundi yaliyolengwa juu ya mabadiliko. Wanufaikaji wanapaswa kuchaguliwa kupitia michakato ya wazi na wanapaswa kupata hakimiliki zenye uhakika zilizoko katika nyaraka za umma. Njia za utatuzi wa migogoro zinapaswa kuwepo kwa mujibu wa sheria zilizopo. Pia, Serikali zinapaswa kujitahidi kuzuia ufisadi katika miradi ya mabadiliko ya ugawaji hususani kupitia uwazi na ushirikishwaji wa kiwango cha juu.

15.10 Kwa kuzingatia ushirikishwaji wa wadau wote, Serikali zinapaswa kusimamia na kutathmini matokeo ya miradi ya mabadiliko ya ugawaji ikiwa ni pamoja na sera zinazohusika kutoa msaada kama zilivyoorodheshwa katika aya ya 15.8, na madhara juu ya upatikanaji wa ardhi na uhakika wa chakula kwa wanaume na wanawake na, inapolazimu, Serikali zinapaswa kuchukua hatua za kurekebisha.

## 16. Utwaaji Ardhi na Fidia

16.1 Kwa kutegemea sheria za kitaifa na utungaji sheria na kwa muktadha wa kitaifa, Serikali zitwae ardhi, pale tu ambapo haki za ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu zinahitajika kwa matumizi ya umma. Serikali ifafanue kwa usahihi dhana ya matumizi ya umma kisheria, ili kuruhusu marekebisho kupitia mahakama. Serikali zihakikishe kwamba matendo yote yanalingana na sheria za kitaifa na pia majukumu yaliyopo chini ya sheria za kitaifa na kimataifa, na kwa kuzingatia ahadi za hiari zilizoko katika nyenzo zinazotumika kitaifa na kimataifa. Serikali ziheshimu wamiliki wote wa hakimiliki halali, hasa wanaotoka kwenye makundi yaliyohatarini na yaliyotengwa, kwa kujipatia rasilimali ndogo na muhimu inayohitajika na kutoa fidia kwa haraka kwa mujibu wa sheria za taifa.

16.2 Serikali zihakikishe kwamba mipango na mchakato wa kutwaa ardhi zipo wazi na ni shirikishi. Yeyote ambaye anaweza kuathirika atambulike, na ataarifiwe kwa namna inayofaa na kushirikishwa katika kila hatua. Mashauri, kulingana na kanuni za mwongozo huu, yatoe taarifa kuhusiana na njia mbadala zinazowezekana kufikia lengo la umma, na zizingatie mikakati ya kupunguza usumbufu katika shughuli za kujiingizia kipato. Serikali ziwe makini, pale ambapo utwaaji wa ardhi utahusisha maeneo muhimu ya utamaduni fulani, dini, au mazingira, au pale ardhi, maeneo ya

uvuvi na misitu ina umuhimu hasa kwa shughuli za kujiingizia kipato kwa watu maskini au walio hatarini.

16.3 Serikali zihakikishe uthamini wa haki na fidia kwa haraka kwa kufuata sheria za nchi. Pamoja na taratibu nyingine, fidia inaweza kuwa, kwa mfano, pesa taslimu, haki ya kupewa ardhi mbadala, au vyote.

16.4 Kwa kiwango ambacho rasilimali zinaruhusu, Serikali zihakikishe kwamba wakala za utendaji zina uwezo wa watumishi, vitendea kazi, fedha na aina zingine za uwezo.

16.5 Pale ambapo ardhi, maeneo ya uvuvi, na misitu haihitajiki tena kutokana na kubadilika kwa mipango, Serikali ziwape wamiliki halali wa mwanzo nafasi ya kwanza kumiliki tena rasilimali hizi. Katika hali kama hii upatikanaji mpya wa ardhi uzingatie kiasi cha fidia kilichopokelewa kwa malipo ya utwaaji ardhi.

16.6 Pande zote ziendelee kupambana na ufisadi, hasa kwa ukadiriaji thamani bila upendeleo, uwazi na utaratibu wa ugatuzi wa michakato na huduma, na haki ya kukata rufaa.

16.7 Pale ambapo uondoaji watu kwa nguvu unafikiriwa kuhalalishwa kwa matumizi ya umma, kama matokeo ya utwaaji wa ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu, Serikali zifanye uondoshaji huo kwa kuwatendea vyema wote waliooathirika kwa namna inayoendana na majukumu yao yanayohusiana na kuheshimu, kulinda, na kutimiza haki za binadamu.

16.8 Kabla ya uondoaji watu au kubadilisha matumizi ya ardhi, ambayo yanaweza kusababisha kuwanyima watu binafsi na jamii fursa ya kupata rasilimali zao za uzalishaji, Serikali ifanye uchunguzi mbadala kwa kukusanya maoni kutoka kwa walioathiriwa, kulingana na kanuni za Mwongozo huu, ukiwa na mwelekeo wa kuepuka au angalau kupunguza, haja ya kukimbilia uondoaji watu kwa kutumia nguvu.

16.9 Shughuli za uondoshaji na uhamishaji zisisababishe mtu kuachwa bila mahali pa kuishi au bila kulindwa dhidi ya ukiukwaji wa haki za binadamu. Pale ambapo wale walioathirika wanashindwa kujihudumia, Serikali, kwa kiwango ambacho rasilimali zinaruhusu, zichukue hatua stahiki kutoa nyumba mbadala, kuwapa makazi mapya, au upatikanaji wa ardhi ya uzalishaji, maeneo ya uvuvi na misitu, kwa kutegemea na hali itakavyokuwa.

# Sehemu ya Tano 5

## Usimamizi wa Miliki

Sehemu hii inahusu usimamizi wa miliki za ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu kwa kwa mujibu wa kumbukumbu za hakimiliki, ukadiriaji wa thamani, utozaji kodi, upangaji wa maeneo unaodhibitiwa, utatuzi wa migogoro juu ya miliki na masuala yanayohusisha mipaka ya nchi zaidi ya moja.

### 17. Kumbukumbu za hakimiliki

17.1 Serikali inapaswa kuweka mifumo (kama vile mifumo ya usajili, utambulishaji wa mipaka na mifumo ya utoaji leseni) ili ya kumbukumbu za hakimiliki za mtu mmojammoja au za pamoja ili kuboresha usalama wa hakimiliki, ikiwamo zile zinazosimamiwa kwa ubia kati ya serikali na sekta binafsi, sekta binafsi, jamii asilia, na wazawa pamoja na watu wa jamii zingine kwa kutumia mfumo wa kitamaduni wa hakimiliki; na kwa ajili ya shughuli za jamii za eneo husika na za masoko. Mifumo hiyo iweke kumbukumbu, kuendeleza na kueneza hakimiliki na majukumu yake, ikiwamo taarifa ya wale wanaohodhi haki hizo na majukumu, sehemu au umilikaji wa ardhi, maeneo ya uvuvi au misitu pamoja haki na wajibu za wanaohusika.

17.2 Serikali zinapaswa kuweka mifumo ya utunzaji kumbukumbu inayofaa kwa mazingira maalumu, ikiwamo wafanyakazi na fedha zilizopo. Njia za kijamii na kiutamaduni zinazofaa kuweka kumbukumbu za wazawa na watu wa jamii zingine zenye mifumo ya kiutamaduni za umilikishaji zinapaswa kuendelezwa na kutumika. Ili kuimarisha uwazi na ulinganifu wa vyanzo vingine vya taarifa za maeneo na malengo mengine, Serikali ihakikishe inatengeneza mfumo shirikishi utakaohusisha mifumo iliyopo ya uwekaji kumbukumbu na mifumo mingine ya taarifa za maeneo ya ardhi. Katika kila eneo la kiutawala, kumbukumbu za hakimiliki za serikali na sekta binafsi, na wazawa na watu wa jamii zingine zenye mifumo ya kitamaduni ya umilikishaji inapaswa kuhifadhiwa katika mfumo jumuishi. Pale ambapo haiwezekani kuweka kumbukumbu za haki za miliki za jamii asili, wazawa na jamii zingine zenye mifumo ya kiutamaduni, au shughuli za kipato katika makazi yasiyo rasmi, umakini thabiti unapaswa kuchukuliwa ili kuzuia usajili wa haki kinzani kwenye maeneo hayo.

17.3 Serikali zihakikishe kuwa kila mtu anaweza kuweka kumbukumbu za hakimiliki na kupata taarifa bila ubaguzi kwa kigezo chochote. Inapofaa, mamlaka za utendaji, kama vile masijala ya ardhi, zianzishe vituo vya utoaji huduma au ofisi zinazohamishika, kwa kuzingatia ufikiwaji wa wanawake, watu masikini na makundi maalumu. Serikali zinapaswa kufikiria kuwatumia wataalamu wa eneo hilo kama vile wanasheria, wahakiki nyaraka, wapima ardhi (soroveya), na wanasayansi jamii kufikisha taarifa za hakimiliki kwa umma.

17.4 Taasisi za utekelezaji zitumie taratibu zilizorahisishwa na teknolojia stahiki kwa sehemu zinazohusika ili kupunguza gharama na muda unaohitajika katika upatikanaji wa huduma. Usahihi wa maeneo na vipande vingine vya ardhi utoshe kama ushahidi ili kukidhi mahitaji ya maeneo hayo, kama utahitajika. Kuwezesha utumiaji wa kumbukumbu za hakimiliki, taasisi za utekelezaji hazina budi ziunganishe taarifa za hakimiliki, wamiliki wa haki hizo, na vipande vya ardhi (eneo) vinavyohusika na haki hizo. Kumbukumbu ziwekwe kwa mpangilio maalumu wa vipande vya ardhi na wamiliki wa haki hizo ili kuruhusu haki kinzani au zinazopishana na za sehemu hizo ziweze kuainishwa.

Kama sehemu kubwa ya upashanaji taarifa, kumbukumbu za hakimiliki zipatikane kwa Serikali za mitaa ili kuboresha huduma zao. Taarifa zitolewe kwa mujibu wa viwango vya kitaifa, na zihusishe taarifa kuhusu hakimiliki zilizonyambulishwa.

17.5 Serikali zihakikishe kuwa taarifa za hakimiliki zinapatikana kwa urahisi kwa wote, kutegemeana na vizuizi vya usiri vilivyoko. Vizuizi kama hivyo visizuie bila sababu ya msingi uchunguzi wa umma katika kutambua ufisadi na shughuli zisizo halali. Serikali na wadau wengine wajitahidi kuzuia ufisadi katika uwekaji kumbumbu za hakimiliki kupitia matangazo mengi kuhusu mahitaji, tozo na misamaha yoyote, na tarehe za mwisho za upatikanaji wa maombi ya huduma inayoombwa.

## 18. Uthamini

18.1 Serikali zihakikishe mifumo sahihi inatumika katika kuthamini hakimiliki kwa usawa na kwa wakati, kwa malengo mahususi, kama vile utendaji wa masoko, udhamini wa mikopo, shughuli za hakimiliki kama matokeo ya uwekezaji, utwaaji na ulipaji kodi. Mifumo hiyo ihamasishe malengo mapana na endelevu ya kijamii, kiuchumi, kimazingira na malengo ya maendeleo endelevu.

18.2 Sera na sheria zinazohusiana na uthamini zijitahidi kuhakikisha kuwa mifumo ya uthamini inazingatia thamani halisi ya tunu zisizo na masoko, kama vile kijamii, kitamaduni, kidini, kiroho na kimazingira pale inapowezekana.

18.3 Serikali inapaswa kutengeneza sera na sheria zinazohamasisha na kuhitaji uwazi katika kuthamini hakimiliki. Bei ya mauzo na taarifa kama hizo ziwekwe kumbukumbu, zichambuliwe na zipatikane ili kuweka msingi sahihi ya ukadiriaji wa thamani za kuaminika na uhakika.

18.4 Serikali na wadau wengine waandae na kutangaza viwango vya kitaifa vya uthamini kwa ajili ya serikali, biashara na matumizi mengine. Viwango vya kitaifa viendane na viwango vya kimataifa. Mafunzo kwa wafanyakazi yahusishe mbinu na viwango vya kimataifa.

18.5 Taasisi za utendaji ziweke taarifa zake za uthamini na uchambuzi kwa umma kwa kuzingatia viwango vya kitaifa. Serikali ziendelee kuzuia ufisadi katika uthamini kwa kufuata uwazi kwenye taarifa na mbinu zinazotumika, katika utawala wa rasilimali za umma na utoaji fidia, na katika hesabu za kampuni na ukopeshaji.

## 19. Utozaji Kodi

19.1 Serikali zina uwezo wa kuongeza mapato kupitia kodi zinazohusiana na hakimiliki ili kuchangia katika mafanikio ya malengo yake mapana ya kijamii, kiuchumi, na kimazingira. Malengo haya yanaweza kuhusisha uhamasishaji wa uwekezaji au uzuiaji madhara yasiyopendelewa yanayoweza kujitokeza kama vile kutokuwa na uhakika wa mmiliki halali na wamiliki wengi au haki zingine za kumiliki. Kodi zihamasishe tabia chanya za kijamii, kiuchumi na kimazingira, kama vile kuweka wazi shughuli zote zinazofanyika na kutangaza thamani ya mauzo yote.

19.2 Serikali zihakikishe zinaandaa sera, sheria na mifumo ya usimamizi itumike kwa ajili ya kudhibiti aina zote za kodi kwenye hakimiliki. Sera na sheria za kodi zitumike inapofaa ili kutoa msaada madhubuti wa kifedha kwa Serikali za ngazi ya chini zilizogatuliwa madaraka na utoaji huduma katika jamii hizo na miundombinu.

19.3 Serikali zisimamie kodi kwa ufanisi na uwazi. Watendaji wa taasisi za utekelezaji wapewe mafunzo yanayojumuisha njia za utendaji. Kodi zizingatie thamani halisi. Ukadiriaji wa thamani na viwango vya kodi viwekwe wazi kwa umma. Serikali ziwape walipa kodi haki ya kukata rufaa dhidi ya uthamini. Serikali ziendelee kuzuia ufisadi katika usimamizi wa

kodi, kwa kuimarisha uwazi katika matumizi yakinifu ya thamani zilizokadiriwa.

## 20. Udhibiti wa Maeneo Yanayopangwa

20.1 Udhibiti wa maeneo yanayopangwa unaathiri hakimiliki kwa kudhibiti matumizi yake kisheria. Serikali ziratibu maeneo yanayodhibitiwa, nazifuatilie utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi, ikiwamo, kuzingatia pande zote katika uwekaji mipaka endelevu, katika namna ambayo itaimarisha malengo ya Miongozo hii. Kwa kuzingatia hili, upangaji wa maeneo upatanishe na kuunganisha malengo tofauti ya matumizi ya ardhi, uvuvi na misitu.

20.2 Serikali ziandae kupitia ukusanyaji maoni na ushiriki, na zitangazie umma, sera zinazozingatia jinsia na sheria juu ya udhibiti wa uratibu wa maeneo yaliyopangwa. Inapofaa, mifumo rasmi ya upangaji wa maeneo izingatie njia za upangaji na uendelezaji wa mipaka zinazotumika na wenyeji wa eneo hilo na jamii nyinginezo zenye mifumo ya kitamaduni ya hakimiliki, na taratibu za utoaji uamuzi ndani ya jamii hizo.

20.3 Serikali zihakikishe kwamba upangaji wa maeneo yanayoratibiwa unafanyika kwa namna ambayo inatambua uhusiano wa mwingiliano uliopo baina ya ardhi, maeneo ya uvuvi, na misitu na matumizi yake, ikijumuisha matumizi yanayozingatia jinsia.Serikali zijitahidi katika kufikia makubaliano na kutoa kipaumbele kwa umma, jamii na matarajio binafsi na kuzingatia masharti ya matumizi mbalimbali kama vile vijiji, kilimo, wahamiaji, miji na mazingira. Upangaji wa maeneo uzingatie hakimiliki zote, pamoja na zile zinazokinzana na za eneo mahususi na hakimiliki za muda maalumu. Tathmini ya hatari ifanyike kwa ajili ya upangaji wa maeneo. Upangaji wa maeneo kitaifa, kikanda na mahali mahususi uratibiwe

20.4 Serikali zihakikishe kwamba kuna ushiriki mpana wa wananchi katika mapendekezo na uhakiki wa rasimu ya upangaji wa maeneo na mapitio ya mpango kuhakikisha kwamba vipaumbele na matarajio ya jamii, ikiwamo wazawa na watu wa jamii za wazalishaji chakula zinaangaliwa. Inapobidi, jamii ziwezeshwe wakati wa mchakato wa upangaji maeneo. Taasisi za utendaji zionyeshe namna ambavyo michango ya wananchi kutoka katika ushirikishwaji wao imefanyiwa kazi katika mipango ya mwisho ya upangaji ardhi. Serikali iendelee kuzuia ufisadi kwa kuanzisha ulinzi dhidi ya matumizi mabaya ya mamlaka katika upangaji ardhi, hasa kuhusiana na mabadiliko katika matumizi yaliyodhibitiwa. Taasisi tendaji zitoe taarifa kuhusu ufuatiliaji wa matokeo.

20.5 Upangaji maeneo uzingatie mahitaji ya kukuza utofauti wa uangalizi endelevu wa ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu, pamoja na mbinu za kilimo kinachozingatia viumbe na mazingira na mkazo endelevu, na kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi na usalama wa chakula.

## 21. Utatuzi wa Migogoro ya Hakimiliki

21.1 Serikali ziwezeshe kupitia vyombo huru, halali na visivyoegemea upande wowote vya kimahakama na taasisi za kiutawala upatikanaji wa njia madhubuti za kutatua migogoro kuhusu hakimiliki kwa wakati na kwa gharama nafuu, pamoja na njia mbadala za kutatua migogoro hiyo, na zinapaswa kutoa hukumu na zenye haki ya kukata rufaa. Hukumu hizo zinapaswa kutekelezwa kwa haraka. Serikali zinapaswa zitoe kwa watu wote, taratibu za kuepusha migogoro au kuitatua katika hatua za awali, ama ndani ya taasisi za utekelezaji au nje. Huduma za utatuzi wa migogoro ziwafikie watu wote, wanawake na wanaume, kwa kuzingatia maeneo waliko, lugha na taratibu zilizowekwa.

21.2 Serikali zinaweza kufikiria kuanzisha mahakama maalumu au vyombo ambavyo vitashughulikia kwa upekee migogoro ya hakimiliki na kuandaa mitazamo ya kitaalamu katika mamlaka za kisheria kwa ajili ya kushughulikia masuala ya kiufundi. Serikali zinaweza pia kufikiria kuwa na mabaraza maalumu ya kushughulikia migogoro inayotokana na upangaji wa maendeleo, upimaji wa ardhi na utathmini.

21.3 Serikali ziboreshe na kuendeleza njia mbadala za kutatua migogoro hasa katika ngazi za chini. Pale ambapo kuna taratibu za kimila za kutatua migogoro, zinapaswa kutoa njia za kutatua migogoro ya hakimiliki kwa haraka, haki, zinazofikika, zenye kuaminika, na zisizokuwa za kibaguzi.

21.4 Serikali zinaweza kufikiria kutumia mamlaka za utendaji kutatua migogoro iliyopo ndani ya uwezo wao kitaaluma kama wale wanaojihusisha na upimaji wa ardhi ili kutatua migogoro ya mipaka kati ya vipande vya ardhi ndani ya muktadha wa kitaifa. Uamuzi uwasilishwe kwa maandishi na kwa kuzingatia hoja zisizo na upendeleo, na inapaswa kuwapo na haki ya kukata rufaa kwa vyombo vya mahakama.

21.5 Serikali ziendelee kuzuia ufisadi katika hatua za utatuzi wa migogoro.

21.6 Katika mchakato wa utatuzi wa migogoro, Serikali zijitahidi kuhakikisha zinatoa msaada wa kisheria kwa makundi yasiyo salama na yaliyotengwa kuhakikisha upatikanaji salama wa haki kwa wote bila ubaguzi. Mamlaka

za mahakama na vyombo vingine vihakikishe kuwa wafanyakazi wake wana stadi na umahiri unaohitajika katika kutoa huduma hizo.

## 22. Masuala ya mipaka ya kimataifa

22.1 Serikali zishirikiane, katika mfumo wa namna inayofaa na kwa kushirikisha wadau walioathiriwa, katika kushughulikia masuala ya hakimiliki yanayohusiana na ardhi, maeneo ya uvuvi, na misitu ambayo yanavuka mipaka ya Taifa. Serikali zihakikishe kuwa hatua zote zinaendana na majukumu yaliyopo katika sheria za kitaifa na kimataifa, na kwa kuzingatia ahadi za hiari kwa mujibu wa nyenzo zilizoko za kikanda na kimataifa. Katika nchi ambazo masuala ya mipaka yanayohusiana na hakimiliki yanaibuka, wahusika wote washirikiane kulinda hakimiliki hizo, maisha na uhakika wa chakula kwa watu wanaohamahama wanapokuwa katika mipaka inayofahamika.

22.2 Serikali na watu wengine wachangie katika kuleta uelewa wa masuala ya hakimiliki na mipaka inayoathiri jamii, kama vile, maeneo ya kuchungia au njia za wafugaji za kupitishia mifugo za msimu, na maeneo ya uvuvi ya wavuvi wadogowadogo, yanayovuka mipaka ya taifa linalohusika.

22.3 Inapofaa, serikali iwianishe viwango vya sheria vya utawala wa hakimiliki, kwa mujibu wa majukumu yaliyopo chini ya sheria za kitaifa na kimataifa, na kwa kuzingaatia ahadi za hiari zilizoko katika nyenzo zijulikanazo kitaifa na kimataifa. Inapofaa, hili liratibiwe na vyombo vya kikanda na pande zinazoathirika. Serikali, kwa ushirikiano na pande zinazoathirika kama itafaa, zitengeneze au kuimarisha masharti ya kimataifa yaliyopo katika kusimamia hakimiliki ambazo zinavuka mipaka ya kimataifa. Inapofaa, usimamizi uratibiwe na vyombo vya kikanda. Hili lifanyike hasa kulinda shughuli za kujiingizia kipato na, sambamba na aya ya 4.8, kuhusu haki za wote walioathirika.

# Sehemu ya Sita 6

## Kukabaliana na Mabadiliko ya Tabianchi na Dharura

Sehemu hii inahusu usimamizi wa miliki za ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu katika muktadha wa mabadiliko ya tabianchi, majanga ya asili na migogoro.

### 23. Mabadiliko ya Tabianchi

23.1 Serikali zinapaswa kuhakikisha kwamba hakimiliki halali za ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu za watu wote, jamii zote au watu ambao wanaweza kuathiriwa hasa wakulima, wazalishaji wadogo wa chakula, na watu wanaoishi katika mazingira magumu na waliokandamizwa, zinaheshimiwa na kulindwa na sheria, sera, mikakati na shughuli zinazofanyika kwa lengo la kuzuia na kutatua madhara ya mabadiliko ya tabianchi kwa kuzingatia majukumu, kama ipasavyo, ya mifumo sahihi ya makubaliano juu ya mabadiliko ya tabianchi.

23.2 Pale panapohitajika, Serikali zinapaswa kujitahidi katika kuandaa na kutekeleza mikakati na shughuli hizo kwa kuwashirikisha watu wote, wanawake na wanaume, wanaoweza kuhamishwa kutokana na mabadiliko ya tabianchi. Aidha, utoaji wa ardhi mbadala, maeneo ya uvuvi na misitu, na shughuli za kujikimu kwa watu watakaohamishwa zisiathiri hali ya kiuchumi na maisha ya watu wengine kwa jumla. Vilevile, serikali zinaweza kutoa msaada maalumu kwa visiwa vidogo na mamlaka zingine zinazoendelea.

23.3 Serikali zinapaswa kuwezesha ushirikishwaji wa watu wote na jamii zote katika maafikiano na utekelezaji wa programu za kukinga na kukabili mabadiliko ya tabia ya nchi zikitilia mkazo jamii za wakulima, wazalishaji wadogo wa chakula, na watu wanaoishi katika mazingira magumu na waliokandamizwa ambao wana hakimiliki halali kwa mujibu wa taratibu za ushauri na ushirikishwaji wa Miongozo hii.

### 24. Majanga asilia

24.1 Wadau wote wanapaswa kuhakikisha kwamba masuala ya miliki za ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu yanashughulikiwa wakati wa kuzuia na kujiandaa kuyakabili majanga ya asili. Mifumo ya kisheria ya umiliki,

ikijumuisha upangaji wa matumizi ya ardhi, inapaswa kufanyika ili kuzuia au kupunguza madhara yanayotokana na majanga ya asili.

24.2 Serikali zinapaswa kuhakikisha kwamba shughuli zote zinafanywa kwa kuzingatia majukumu yake kwa mujibu wa sheria za kitaifa na kimataifa yaliyopo na kwa kwa kuzingatia matamko ya hiari ya vyombo vya kikanda na kimataifa. Wadau wote wanapaswa kutenda kwa kuzingatia taratibu za kimataifa ikiwa ni pamoja na Kanuni za Umoja wa Mataifa juu ya Fidia ya Mali kwa Wakimbizi na Watu Waliohamishwa ("Kanuni za Pinheiro"), na Mkataba wa Misaada ya Kibinadamu na Viwango vya Kimsingi vya Kukabiliana na Majanga.

24.3 Serikali zinapaswa kushughulikia umiliki katika programu za kukabiliana na majanga ya asili. Taarifa za hakimiliki halali za maeneo yanayoweza kuathirika zinapaswa kukusanywa kwa kuzingatia kanuni za mashauriano na ushirikishwaji wa Miongozo hii. Mifumo ya kurekodi hakimiliki halali iwe nyumbufu kwa ajili ya majanga ya asili, inayojumuisha utunzaji wa nje wa taarifa ili kuwaruhusu wamiliki halali kuthibitisha haki juu ya ardhi zao na maeneo menginePia, Serikali zinapaswa kujitahidi kutambua maeneo yanayofaa kwa uhamishaji wa muda wa waathirika wa majanga ya asili, na taratibu za utoaji wa usalama wa miliki za maeneo hayo zinapaswa kuandaliwa.

24.4 Serikali na wadau wengine wanapaswa kushughulikia usimamizi wa umiliki katika hatua ya dharura ya kukabili majanga ya asili. Utoaji wa ardhi mbadala, maeneo ya uvuvi na misitu, na shughuli za watu watakaohamishwa zisiingilie haki na shughuli za watu wengine. Hakimiliki halali za watu watakaohamishwa zinapaswa kutambuliwa, kuheshimiwa na kulindwa. Taarifa za hakimiliki halali na matumizi ya ardhi yasiyo halali zinapaswa kufahamika kwa waathirika wa majanga ya asili.

24.5 Serikali na wadau wengine wanapaswa kushughulikia miliki wakati wa hatua za ujengaji upya wa makazi. Watu ambao walihamishiwa katika maeneo ya hifadhi kwa muda wanatakiwa kusaidiwa kwa hiari, kwa usalama na kwa utu wanaporejea katika maeneo yao ya awali. Njia za usuluhishi wa migogoro juu ya masilahi ya hakimiliki zinapaswa kuwekwa. Pale ambapo mipaka ya maeneo binafsi na ya matumizi mengine ya ardhi inapotakiwa kuwekwa, utekelezaji unapaswa kukidhi kanuni za mashauriano na ushirikishwaji za Miongozo hii. Watu wanaposhindwa kurejea katika maeneo yao ya awali, wanaweza kuhamishiwa katika maeneo mengine. Uhamishaji huo unapaswa kujadiliwa na kuidhinishwa na jamii itakayopokea wanaohamishwa ili kuhakikishwa kuwa

wanaohamishwa wana uhakika wa kupata ardhi mbadala, maeneo ya uvuvi na misitu, na shughuli zinginezo bila kuathiri haki na riziki za watu wengine.

## 25. Migogoro Inayohusiana na Umiliki wa Ardhi, Maeneo ya Uvuvi na Misitu

25.1 Wahusika wote wanapaswa kuchukua hatua ili kuzuia kabisa masuala yanayohusu hakimiliki za ardhi, maeneo ya uvuvi, na misitu kuwa chanzo cha migogoro na kuhakikisha kuwa masuala kuhusu hakimiliki yanashughulikiwa kabla ya mgogoro kutokea, wakati wa mgogoro na baada ya mgogoro, ikijumuisha katika hali ambapo maeneo yanakaliwa. Katika hali hiyo, pande zote zitapaswa kutenda kwa mujibu wa sheria zilizopo za kimataifa za haki za binadamu.

25.2 Serikali zinapaswa kuhakikisha matendo yote yanafungamana na majukumu yaliyopo katika sheria za kitaifa na kimataifa, na kwa kuzingatia matamko ya hiari ya nyenzo zinazotumika kikanda na kimataifa. Aidha, inapofaa matendo yajumuishe makubaliano yanayohusiana na hali ya wakimbizi na itifaki zake, na misingi ya Umoja wa Mataifa juu ya urejeshwaji wa nyumba na mali kwa wakimbizi na watu waliokosa makazi (" Kanuni za Pinheiro"). Wakati migogoro ikiendelea na baada ya migogoro kutatuliwa, Serikali zinapaswa kuheshimu sheria za kimataifa za haki za binadamu zinazohusika na hakimiliki halali.

25.3 Ili kuhakikisha matatizo yanayohusu hakimiliki hayasababishi migogoro, wahusika wote wajitahidi kutatua matatizo hayo kwa njia ya maelewano. Serikali zinapaswa kurejelea upya sera na sheria zinazohusika ili kuondoa ubaguzi na sababu zingine zinazoweza kuwa chanzo cha migogoro. Pale inapofaa, Serikali zifikirie kutumia njia za kimila na desturi za eneo linalohusika katika utatuzi wa haraka wa migogoro inayohusu hakimiliki za ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu. Njia hizo ziwe za haki, zinazozingatia usawa, zinazoaminika, zinazozingatia usawa wa kijinsia, na kupatikana bila kubagua.

25.4 Migogoro inapotokea, Serikali na wahusika wengine wajitahidi kuheshimu na kulinda hakimiliki halali zilizopo na kuhakikisha kwamba hazivurugwi na wahusika wakinzani. Kwa kuzingatia wajibu kwa sheria zinazohusika za kitaifa na kimataifa, Serikali hazipaswi kutambua hakimiliki za ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu zilizopatikana chini ya mamlaka yake kwa kutumia mabavu na njia ambazo sio za haki au sahihi. Wakimbizi, watu wengine wasio na makazi pamoja na wengine walioathiriwa na migogoro wanapaswa kupelekwa kwenye maeneo yaliyo salama kwa namna zitazolinda hakimiliki za jamii wenyeji. Ukiukwaji wa hakimiliki uhifadhiwe

kimaandishi, na pale itakapofaa, kurekebishwa. Kumbukumbu rasmi za hakimiliki zinapaswa kulindwa dhidi ya uharibifu wowote na wizi kwa minajili ya kuzitumia kama ushahidi katika michakato ya kushughulikia ukiukwaji wa haki na kufanikisha hatua za kurekebisha ukiukwaji huo. Katika maeneo ambayo hakuna kumbukumbu, hakimiliki zilizopo zinapaswa kuhifadhiwa kwa maandishi kwa namna zitakazofaa zaidi kwa kuzingatia usawa wa kijinsia, pamoja na ushuhuda na historia simulizi. Hakimiliki halali za wakimbizi na watu waliolazimika kuondoka kwenye makazi yao zinapaswa kutambuliwa, kuheshimiwa na kulindwa. Taarifa juu ya hakimiliki na matumizi yasiyoidhinishwa zisambazwe kwa watu wote walioathirika.

25.5 Katika hali ya migogoro, pale inapowezekana au migogoro inapokuwa imekwisha, Serikali na wahusika wengine wanapaswa kuhakikisha matatizo ya hakimiliki yanashughulikiwa kwa namna ambayo itachangia usawa wa kijinsia na kuwezesha upatikanaji wa suluhisho la kudumu kwa wale walioathirika. Pale inapowezekana na inafaa kuwarejesha walioathirika katika hali yao, kwa msaada wa Shirika la Umoja wa Mataifa la kuwahudumia wakimbizi na wakala zingine,wakimbizi na watu waliolazimika kuondoka kwenye makazi yao wanapaswa kusaidiwa kurudi katika maeneo ya asili kwa hiari, usalama, na kwa kuzingatia utu wa mwanadamu kulingana na viwango vya kimataifa. Taratibu za kuwarudisha katika hali zao za awali na ukarabati zisiwe za kibaguzi, bali zizingatie usawa wa kijinsia na kutangazwa kwa mapana. Aidha, madai yanayohusu kurejeshwa katika hali zao za awali yashughulikiwe kwa haraka iwezekanavyo. Taratibu za kurejeshewa hakimiliki za watu asilia na jamii zingine zenye mifumo ya hakimiliki za kimila ziwezeshe matumizi ya vyanzo vya taarifa asilia.

25.6 Pale ambapo urejeshaji wa hali ya awali ya walioathirika hauwezekani, utolewaji wa ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu mbadala na maeneo ya kuishi kwa wakimbizi na watu waliolazimika kuondoka kwenye makazi yao unapaswa kujadiliwa na jamii wenyeji pamoja na washirika wengine wanaohusika ili kuhakikisha kuwa makazi mapya kwa walioathirika hayahatarishi maisha ya wengine. Ikiwezekana, kuwe na taratibu maalumu za kuyapa makundi maalumu yanayojumuisha wajane na yatima, uhakika wa kupata ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu.

25.7 Pale inapofaa, sera na sheria zirejelewe ili kushughulikia upendeleo uliokuwapo na vilevile upendeleo uliojitokeza wakati wa mgogoro. Inapofaa au kuhitajika, wakala zinazohusika zianzishwe upya ili kutoa huduma muhimu kwa usimamizi wa hakimiliki wenye uwajibikaji.

# Sehemu ya Saba 7

## Ukuzaji, Utekelezaji, Ufuatiliaji na Tathmini

26.1 Kwa kuwa Miongozo hii ni ya hiari, Serikali zina jukumu la kuikuza, kuitekeleza, kuifuatilia na kuitathmini.

26.2 Serikali zinahimizwa kuanzisha majukwaa ya wadau na mifumo katika ngazi za mtaa, mkoa, na taifa au kutumia majukwaa na mifumo iliyopo kushirikiana katika utekelezaji wa miongozo hii; kufuatilia na kutathmini utekelezaji wake katika maeneo ya mamlaka yao kisheria, na kutathmini namna ilivyoathiri uboreshaji wa usimamizi wa umiliki wa ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu, na upatikanaji wa chakula kwa uhakika na utambuzi wa haki ya kupata chakula cha kutosha katika muktadha wa kitaifa wa upatikanaji chakula kwa hakika, na maendeleo endelevu. Utaratibu huu unapaswa kuwa jumuishi, shirikishi, uzingatie usawa wa kijinsia, uwe unatekelezeka, wa gharama nafuu na endelevu. Katika kutekeleza majukumu haya, Serikali zinaweza kuomba msaada wa kitaalamu kutoka kwa taasisi za kikanda na kimataifa.

26.3 Wadau wa maendeleo, wakala maalumu za Umoja wa Mataifa na mashirika ya kimataifa yanahimizwa kusaidia jitihada za kujitolea zinazofanywa na Serikali katika kutekeleza Miongozo hii, ikiwemo kupitia ushirikiano miongoni mwa nchi zinazoendelea. Msaada huo unaweza kuwa katika mfumo wa ushirikiano wa kitaalamu, kifedha, kuendeleza uwezo wa taasisi zinazohusika, kuchangia ujuzi na kubadilishana uzoefu katika kuandaa sera za kitaifa za umiliki na ubadilishaji wa teknolojia.

26.4 Kamati ya Umoja wa Mataifa ya Upatikanaji na uhakika wa Chakula itumike kama jukwaa la kimataifa ambapo wadau wanaohusika wanaelimishana kutokana na uzoefu wao, na kutathmini maendeleo yaliyofikiwa katika utekelezaji wa Miongozo hii, na kutumika kwake, uumuhimu wake, na athari zake. Kwa hivyo, Sekretariati ya Kamati ya Upatikanaji wa Chakula kwa kushirikiana na kikundi cha ushauri cha Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa,  ina jukumu la kutoa taarifa kwa Kamati ya Upatikaji wa na uhakika wa Chakula juu ya maendeleo ya utekelezaji wa Miongozo hii. Aidha, vyombo hivi vina wajibu wa kufanya tathmini ya athari na mchango wa Miongozo hii katika kuboresha usimamizi wa umiliki. Ripoti hizi zitolewe kwa nchi zote na

zihusishe, pamoja na vitu vingine, uzoefu katika ngazi ya kikanda na maudhui yaliyojitokeza.

26.5 Wadau wote, yakiwemo mashirika ya kiraia na sekta binafsi, yanahimizwa kutumia mbinu shirikishi kuimarisha na kutekeleza Miongozo hii kwa mujibu wa vipaumbele vya kitaifa na kimuktadha. Aidha, wahusika wote wanahimizwa kueneza taarifa juu ya usimamizi unaowajibika ili kuboresha utekelezaji.

Governance of Tenure

Mwongozo huu ni nyenzo ya kwanza yenye kina na ya kimataifa kuhusu usimamizi wa umiliki iliyoandaliwa kupitia mashauriano ya kiserikali. Ndani mwake mna ufafanuzi wa kanuni na viwango vilivyokubalika kimataifa kuhusu vitendo vyenye uwajibikaji katika matumizi na udhibiti wa ardhi, maeneo ya uvuvi na misitu. Kanuni zilizomo zinatoa mwelekeo wa kuimarisha sera, sheria na taratibu za kiasasi zinazodhibiti haki za umiliki; uendelezaji wenye uwazi na usimamizi bora wa mifumo wa miliki; na kuimarisha uwezo na utendaji kazi wa mashirika ya umma, mashirika binafsi ya uwekezaji, asasi za kiraia, na watu wenye maslahi katika umiliki na usimamizi wa miliki. Miongozo iliyomo humu imejadili usimamizi wa umiliki katika kiwango cha kitaifa kwa ajili ya upatikanaji wa chakula kwa uhakika, na imekusudiwa kuchangia katika upatikanaji, kwa hatua, wa chakula cha kutosha, kutokomeza umaskini, kulinda mazingira na kufanikisha maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi.

www.fao.org/nr/tenure

ISBN 978-92-5-134532-0

9 789251 345320

I2801SW/1/09.21